PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

Jarida la BUNGE

Toleo Maalum la Mkutano wa 153 wa IPU

ISSN-085-6064 TOLEO LA 14 Novemba 2026



Tulia aaga IPU kwa Kishindo! Uk 01

Dkt. Samia ahimiza usimamizi wa rasilimali Uk 13

Bunge la Tanzania lipo tayari kushirikiana na mabunge mengine Uk 25

SPIKA ZUNGU: MAAZIMIO YA MKUTANO WA 153 WA IPU YASIBAKI KWENYE MAKARATASI

YALIYOMO


01 Tulia Aaga IPU kwa Kishindo


05 Arusha yaweka Dira ya Utawala Jumuishi


12 Spika Zungu Asisitiza Dunia Kushirikiana


13 Dkt. Samia Ahimiza Usimamizi wa Rasilimali za Umma


17 Umeitendea haki Afrika



18 Spika Zungu: Tanzania imepiga hatua



20 Ni Wakati Muhimu wa Kutathimini


23 Diplomasia ya Utalii


25 Bunge la Tanzania lipo tayari kushirikiana



29 Uhifadhi wa Mazingira uwe chanzo cha fursa


34 Bunge: Samia ameipa Tanzania heshima



43 IPU 153 na Fursa ya Kubadili Diplomasia kuwa Maendeleo

Dibaji



Ndugu Msomaji,

Nakukaribisha kwenye Jarida la Bunge Toleo la Kumi na Nne, Toleo hili ni maalum kwa ajili ya Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) uliofanyika jijini Arusha kuanzia Oktoba 5 hadi 9 2026, katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha. (AICC).

Jarida hili lina makala na habari mbalimbali kuhusiana na Mkutano huo wa Kimataifa ambao uliwakutanisha Washiriki zaidi ya 2,000 wakiwemo viongozi wa mabunge, wabunge na wawakilishi wa taasisi za kibunge kutoka sehemu mbalimbali za dunia kwa lengo la kujadili utawala bora, demokrasia, haki za binadamu na maendeleo jumuishi.

Kufanyika kwa mkutano huu jijini Arusha, Tanzania, kulitoa fursa ya kuitangaza nchi kimataifa na kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na mataifa mengine.

Aidha, mkutano huo ulichangia katika kukuza utalii na shughuli za kiuchumi jijini Arusha kutokana na uwepo wa wageni kutoka sehemu mbalimbali za dunia.

Kwa ujumla, Mkutano huo ulikuwa fursa ya nchi kuonesha utamaduni wake, uwezo wake wa kuandaa mikutano ya kimataifa na dhamira yake ya kushirikiana na mataifa mengine katika kujenga dunia yenye amani, haki na maendeleo endelevu.

Hivyo nakukaribisha usome habari na makala zinazohusu yale yaliyojiri wakati wa Mkutano huo.

Nakutakia usomaji mwema wa Jarida la Bunge.

Ndugu Baraka Leonard
Katibu wa Bunge.

Bodi ya Uhariri

Mwenyekiti
Ngd. Baraka Leonard

Makamu Mwenyekiti
Ndg. Zuhura Mtatifikolo

Wajumbe
Ndg. Athuman Hussein, ndc
Ndg. Hanifa Masaninga
Ndg. Abdallah Hancha

Mhariri
Ndg. Lawrence Raphaely

Mhariri Msaidizi
Ndg. Debora Sanja

Msanifu Kurasa
Ndg. Henry Mbilinyi

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S. L. P. 941,
40490 Tambukareli,
DODOMA
Simu: +255 26 2322761-5
Nukushi: +255 26 2324218
Barua Pepe: cna@bunge.go.tz

Tulia Aaga IPU kwa Kishindo!

- Ataja mafanikio makuu matano
- Amwagiwa sifa kede kede!

Na. Patson Sobha

Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) aliyemaliza muda wake, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), amewaaga Wajumbe wa IPU kwa hotuba iliyoelezea mafanikio makubwa Matano, huku akimwagiwa sifa nyingi kwa utumishi wake wa miaka mitatu wakati wa Mkutano wa 153 wa IPU uliofanyika Arusha kuanzia tarehe 5 hadi 9 Oktoba, 2026.

Akitoa hotuba yake katika kikao cha tano cha Mkutano huo kilichofanyika katika Ukumbi wa Lake Nyasa, mojawapo ya kumbi za Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC), Dkt. Tulia ametaja mafanikio matano kati ya mengi yaliyopatikana tangu alipochaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani tarehe 27 Oktoba, 2023.



"Niruhusuni kutaja kwa ufupi baadhi ya mafanikio muhimu tuliyopata katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, tumeanzisha kitengo maalumu cha uwajibikaji, kwa sababu nguvu halisi ya IPU iko katika kutafsiri maazimio yake kuwa hatua za kitaifa, tumefanya marekebisho ya sheria na kanuni za IPU ili kuirasimisha nafasi ya Makamu wa Rais wa IPU kama Naibu halisi wa Rais," alisema Dkt. Tulia.

Dkt. Tulia ameyataja mafanikio mengine kuwa ni kutimiza ahadi yake ya kuimarisha sauti za wabunge vijana ndani ya IPU kwa kupunguza umri wa kutambulika kama mbunge kijana kuwa chini ya miaka 40. Aidha, amesema wamefanya marekebisho ya Sheria na Kanuni za IPU ili kuweka usawa wa kijinsia kama lengo lao la pamoja, ambapo sasa wamekaribia kufikia asilimia 40.

Aliyataja mafanikio mengine kuwa ni kuidhinisha Sera ya Kuzuia Unyanyasaji ili kuwalinda wajumbe na watumishi wakati wa mikutano ya IPU. Aidha, amesema anapomaliza kipindi chake cha uongozi, anaondoka akiwa na shukrani nyingi kwani mafanikio hayo sio kwa juhudi zake peke yake bali kwa juhudi za pamoja.

"Ninapomaliza kipindi changu cha uongozi, ninaondoka nikiwa na shukrani nyingi kwa sababu mafanikio yoyote ambayo tumeyapata hayakupatikana kwa juhudi zangu pekee, bali kwa juhudi za pamoja, nanyi mkiwa sehemu yake," alisema Dkt. Tulia.

Akizungumzia Azimio la Mkutano huo wa 153 lililopewa jina la Taarifa Maalum ya Arusha, alisema funzo kuu walilolipata katika mijadala ya siku chache zilizopita ni kwamba utawala bora umefungamana moja kwa moja na uhusiano kati ya wananchi na taasisi zao. Amesema imani ya wananchi ni kipimo kinachoweza kutumika kutathmini hali ya uhusiano huo kwani kwa mujibu wa Mkakati wa IPU uliopitishwa mjini Istanbul ulitambua kupungua kwa imani ya wananchi na kubanwa kwa nafasi ya ushiriki wa kiraia, ikiwemo vitisho dhidi ya wabunge, kuwa miongoni mwa changamoto zinazokabili demokrasia na mabunge duniani leo.

Dkt. Tulia alisema, Azimio lililopitishwa na Mkutano huo, yaani Taarifa Maalum ya Arusha, limekuwa muhimu sana katika wakati huu ambao wanashuhudia kudorora kwa maendeleo ya kidemokrasia duniani, na ambapo wengi wa wajumbe wanatambua kwamba wanasiasa wanazidi kupoteza imani ya wananchi wanaowawakilisha.

"Azimio lililopitishwa na Mkutano huu lililopewa jina la Taarifa Maalum ya Arusha, linakuwa muhimu sana katika wakati ambao tunashuhudia kudorora kwa maendeleo ya kidemokrasia duniani, na ambapo wengi wenu mmetambua kwamba wanasiasa wanazidi kupoteza imani ya wananchi wanaowawakilisha." Aliongeza kusema Dkt. Tulia.

Alisema, Taarifa Maalum ya Arusha inawaalika Wabunge kurejea kwa wananchi wao na hasa ngazi za chini za jamii ili kupata fursa ya kuwasikiliza kwa makini zaidi na kupitia uzoefu wao na udhaifu wa takwimu, kuenea kwa taarifa potofu na za upotoshaji, pamoja na mahitaji ya kuchukua hatua kwa haraka.

Aliongeza kusema kuwa hali hiyo inazidi kuwa ngumu kutokana na kuibuka kwa teknolojia ya akili mnemba ambayo licha ya uwezo na umuhimu wake, inaweza pia kurahisisha kusambaa kwa taarifa za upotoshaji na habari zisizo sahihi.

Rais aliyemaliza muda wake, amesema suluhisho la changamoto zinazoikabili demokrasia ya leo haihitaji kubadili kabisa mifumo ya kisiasa wala kutafuta mbinu ya kimiujiza. Badala yake, Taarifa Maalum ya Arusha inawakumbusha kurejea kwenye chimbuko na misingi ya demokrasia ya uwakilishi ambayo imejengwa juu ya imani ya wananchi. Aliwakumbusha kuwa, imani hiyo haipo daima, ni kitu kinachopatikana kwa juhudi za kila siku katika maisha ya kawaida, mbali na wakati wa uchaguzi ambapo wananchi hujitokeza kupiga kura kila baada ya miaka kadhaa.

Hoja nyingine aliyoizungumzia kuhusiana na azimio hilo ni suala la uwakilishi kwamba hauhusiani tu na kuzungumza kwa niaba ya wananchi, bali kuhakikisha kuwa maisha na uhalisia wao vinaongoza maamuzi yanayofanyika katika vyombo vya kutunga sheria. Dkt. Tulia amesema, mwakilishi wa wananchi anapaswa kuhakikisha kuwa sheria, bajeti na shughuli za usimamizi zinadhihirisha uzoefu, matarajio na changamoto halisi za jamii anayoitumikia.

Mheshimiwa Dkt. Tulia akizungumzia uwajibikaji na uadilifu, alisema ni mahitaji ya msingi ya demokrasia kama ilivyoainishwa kwenye Taarifa Maalum ya Arusha. Aidha, alisema taasisi za kisiasa ambazo haziwajibishwi zinapoacha kutumikia maslahi ya umma haziwezi kuaminiwa, na hapo ndipo demokrasia hudhoofika na jamii zetu kuwa



rahisi kuathiriwa na migawanyiko, hatari ya kuvunjika kwa amani na kuzuia maendeleo ya jamii.

Hoja nyingine inayoendana kikamilifu na mkakati wa IPU aliyoizungumzia ni kuyafanya mabunge kuwa wazi na jumuishi zaidi, ili kuakisi jamii zinazowakilishwa; wakiwemo wanawake na wanaume, vijana na wazee, watu wenye ulemavu, wahamiaji, wakimbizi, watu wasio na uraia, jamii za vijijini, maeneo ya pembezoni mwa miji, pamoja na makundi yote ambayo kwa muda mrefu yamesahaulika katika michakato ya kufanya maamuzi.

Aidha, alisema kuwa mabunge lazima yazuie rushwa, yadumishe uadilifu, yaimarishe wajibu wake wa usimamizi na yaoneshe kwamba ushiriki wa wananchi unaweza kuleta mabadiliko yanayoonekana. "Wananchi lazima waone kuwa wanapozungumza, wanasikilizwa na kwamba kusikilizwa kwao kunaweza kuleta tofauti katika maisha yao ya kesho," alisema Dkt. Tulia.

Pongezi za Wajumbe

Wakitoa pongezi, shukrani na kueleza sifa za Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kupitia makala maalum ya kumuaga kwa njia ya video, wajumbe wa Mkutano wa 153 wa IPU wakiongozwa na Rais mpya wa 32 na Spika wa Bunge la Australia, Mhe. Milton Dick, wamempa sifa nyingi na shukrani.

Mheshimiwa Milton Dick ambaye alisema anajivunia kumwita Mheshimiwa Dkt. Tulia rafiki yake, anampenda kwa sababu ya tabia yake yenye nguvu na uwezo wa kuleta watu pamoja. Alimshukuru sana kwa jitihada zake kubwa hasa katika suala la kujenga umoja na bidii katika utendaji wake kwa miaka mitatu.

Makamu wa Rais wa IPU ambaye pia ni Seneta wa Seneti ya Poland, Mheshimiwa Gabriela Morawska-Stanecka, alisema katika kufanya kazi na Dkt. Tulia kwa miaka hiyo mitatu, ameguswa sana na jinsi anavyojishusha, anavyofikika kwa urahisi na moyo wake uliojaa wema. Alisema anapenda sana anavyoongoza vikao na kuanza na maneno "wapendwa marafiki zangu na wajumbe wenzangu", pia anavyogonga meza kwa nyundo akihitimisha uamuzi.



Spika wa Bunge la Zambia, Mheshimiwa Nelly Mutti, alisema anampenda sana Dkt. Tulia kwa sababu ana misimamo, anajiamini, ana akili nyingi sana, na ana namna ya kuongea kwa ulaini, lakini yuko imara na ni rahisi kuona uthabiti wake anavyosisitiza jambo. Alisema, Dkt. Tulia sio tu alikuwa Rais wa IPU, bali kwake anamwona zaidi kuwa rafiki wa karibu na dada yake.

Mheshimiwa Mutti, aliendelea kummwagia sifa Dkt. Tulia akisema, wakati wa utumishi wake, amekuza diplomasia ya kimataifa ya kibunge akijikita zaidi katika ajenda za kuzuia mabadiliko ya hali ya hewa, amani, ulinzi na usalama, na masuala ya haki, usawa wa kijinsia, pamoja na kuwainua vijana.

Mbunge wa Chile Mheshimiwa Rojo Edwards, alisema anampenda Mhe. Dkt. Tulia kwa sababu katika uongozi wake hakuwahi kuhitaji kupaza sauti yake sana ili mtu atambue kwamba yuko katikati yao. Aliongoza kwa kujiamini, kwa tabasamu la bashasha na kwa namna hiyo aliweza kuleta watu pamoja kwa urahisi. Aidha, amesema, uchangamfu wake, uwazi, utayari wa kusikiliza na kuelewa misimano ya wengine, ni kipaji cha pekee ambacho watakikosa sana na kukikumbuka daima.

Spika wa Bunge la Azerbaijan Mheshimiwa Sahiba Gafarova, alisema anavutiwa zaidi na uchangamfu wake Dkt. Tulia, uwazi anaouonesha katika kila afanyacho, lakini pia ana uwezo mkubwa wa kuwaunganisha watu na kufanya kila mmoja ajisikie vizuri. Aidha, Kareen Jabre, ambaye ni Mkurugenzi wa Mipango wa IPU, yeye anapenda zaidi mguso





wa kiutu na ubinadamu na nguvu chanya ya uchangamfu aliyonayo Dkt. Tulia.

Naye Katibu wa IPU, Mheshimiwa Balozi Anda Filip kutoka Romania alisema, kikubwa anachompendea Dkt. Tulia ni tabia ya uadilifu wake binafsi na kufuata misingi ya maadili ya uongozi ambavyo vinawapa wengi wao funzo na hamasa. Alisema pia, namna anavyojiweka kama kiongozi vinamfanya awe na muonekano wa heshima. Amemalizia kwa kumshukuru Dkt. Tulia kwa kuifanya IPU kuwa nzuri zaidi.

Mfanyakazi mwingine wa Umoja wa Mabunge Duniani, Thomas Fitzsimons ambaye ni Mkurugenzi wa Mawasiliano wa IPU, alianza kusema kwa utani kwamba anampenda Dkt. Tulia kwa kuwa ni mrefu kuliko yeye, na kuongeza kwa kusema kwamba Dkt. Tulia ni mnyenyekevu na anaheshimu kila mtu ikiwa ni pamoja na watendaji wa Sekretarieti ya IPU, licha ya kuwa yeye ni kiongozi mkubwa na ana wafuasi zaidi ya milioni moja kwenye mtandao wa Instagram.

Wajumbe wengi wa IPU, walielezea sifa nyingi akiwepo Mheshimiwa Laurent Wehrli, ambaye ni Mbunge wa Switzerland aliyesema anampenda Dkt. Tulia kutokana na moyo wake wa kujitoa, kuwa na nguvu ya uamuzi, na uwezo wake wa kuhakikisha kwamba sauti ya IPU inasikika duniani kote. Aidha, Mhe. Claudio Sampaio, Mbunge wa Brazil alisema kwamba pamoja na uongozi wake wa kutumia akili nyingi, diplomasia na uvumilivu kwa wajumbe wote, anapenda namna anavyoongoza kwa utulivu na tabasamu lake murua ambalo ni hamasa kubwa kwa wajumbe na kwamba anaweza

kuleta watu pamoja kwenye mazungumzo na kulenga kupata suluhisho.

Spika wa Bunge la Qatar, Mheshimiwa Dkt. Hamda Bint Hassan Al Sulaiti alisema, kitu atakachobaki nacho kama kumbukumbu ya Mhe. Dkt. Tulia ni imani yake isiyoyumba, misimano yake katika jambo analonuia, uthabiti katika kufikia kile anachokitafuta na kukiamini. Aidha, alisema, Dkt. Tulia hana tabia ya kurudi nyuma kujipanga pale anapokutana na changamoto, badala yake anazikabili kwa kujiamini, busara na roho ya imani ya kufikia mafanikio na kwa uwezo huo ukichanganya na tabia yake ya utu na uchangamfu, ndicho kinamfanya awe kiongozi wa kipekee sana.

Akipokea shukrani na pongezi hizo, Mheshimiwa Dkt. Tulia aliwashukuru wote waliozungumza na kumsemea maneno ya ukarimu kuhusu yeye binafsi na kuhusu uongozi wake. Alisema amepokea kwa unyenyekevu mkubwa na kwa kuridhika, watu wametambua azma yake ya kutimiza ahadi alizotoa miaka mitatu iliyopita alipochaguliwa kushika wadhifa huo wa juu sana.

Pia aliwashukuru kwa dhati wote waliomsindikiza katika safari hiyo akiwemo Katibu Mkuu wa sasa Balozi Anda Filip na Katibu wa zamani ambaye sasa anaitwa Katibu Mkuu wa Heshima, Martin Chungong, Wajumbe wa Kamati Tendaji na Vyombo Maalumu vya IPU, Sekretarieti ya IPU na wasaidizi wake katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Dkt. Tulia, alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na Spika wa Bunge, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, kwa msaada wa kisiasa uliowezesha Mkutano huo Mkuu kufanyika. Aidha, ametoa shukrani za pekee kwa wananchi wa Arusha na Tanzania kwa ukarimu wao wa hali ya juu na kujitolea kwao, jambo ambalo limetambuliwa na wageni kutoka mataifa yote ya IPU.

Dkt. Tulia alisema, anaondoka katika nafasi ya Rais, lakini ataendelea kuwa Balozi wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Alisema kuwa ana uhakika kwamba anaicha nafasi hiyo mikononi mwa mtu mwenye uwezo mkubwa mrithi wake, Mhe. Milton Dick, Spika wa Baraza la Wawakilishi la Australia. Alimtakia kila la heri katika jitihada zake za kuipeleka IPU katika viwango vya juu zaidi.

ARUSHA YAWEKA NA WENYE UWAJ

• Mkutano wa 153 wa IPU waweka Azimi

Na Henry Mbilinyi

Kuna aina ya diplomasia ambayo mara chache huonekana katika habari za vichwa vya magazetini. Si diplomasia inayohusisha mikutano mikubwa ya viongozi au mvutano mkali katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Badala yake, hufanyika katika vyumba vya mikutano ambako wawakilishi waliochaguliwa na wananchi hukaa pamoja na kujadili kila kipengele cha nyaraka rasmi, wakibishana kuhusu mitazamo, fikra na maneno yanayopaswa kutumika.

Hata hivyo, katika kipindi ambacho ushirikiano wa kimataifa unazidi kudhoofika, mikutano hii ni miongoni mwa maeneo machache ambayo dunia bado inaweza kufikia makubaliano na kuzungumza kwa sauti za pamoja.

Kwa siku tano Oktoba 2026, Jiji la Arusha, lililoko kaskazini mwa Tanzania chini ya safu za Mlima Meru, limekuwa kitovu cha diplomasia



KA DIRA YA UTAWALA JUMUISHI AJIBIKAJI

mio la kwanza kuhusu Haki za Walemavu, Mwito kwa Majanga ya Tabianchi.

ya Dunia. Ni makao ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na eneo ambalo mikataba muhimu iliyochangia kuleta amani katika bara hili imekuwa ikijadiliwa.

Zaidi ya wajumbe 2,000 kutoka nchi wanachama 184 walikusanyika katika jiji la Arusha kwa ajili ya Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Miongoni mwao walikuwamo Maspika na Naibu Spika wa mabunge.

Mkutano huu umefanyika wakati dunia ikikabiliwa na changamoto kubwa ikiwa vita vinavyo endelea barani Ulaya na Mashariki ya Kati, Mabadiliko ya Tabianchi, ambayo hapo awali yalionekana kuwa tishio la siku zijazo, lakini sasa imekuwa tatizo halisi linalosababisha madhara makubwa.

Huku taasisi zilizochaguliwa na wananchi katika nchi nyingi zikikabiliwa na shinikizo la mamlaka za utendaji kupanua madaraka yao pamoja na kupungua kwa imani ya wananchi.

katika siku hizo tano, wajumbe walifanikiwa kupata kile ambacho wenyeji wa Tanzania walikiita "lugha ya pamoja." Na kupitisha maazimio ambayo yanajenga matumiani kwa wananchi katika nchi wanachana.

Kuimarisha utawala bora na kuwawezesha wananchi kupitia ushirikishwaji, na fursa kwa wote.

Kama Mkutano huu wa 153 ungepaswa kulipa jina Azimio hili pengine lingeitwa Azimio la Arusha, lenye kichwa Kuimarisha utawala bora na kuwawezesha wananchi kupitia ujumuishi, uaminifu na fursa kwa wote.

Likiwasilishwa katika mkutano mkuu tarehe 9 Oktoba 2026 Mhe. J. A. Chowdhury kutoka Bangladesh na Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro kutoka Tanzania, azimio hili linasomeka zaidi kama ukumbusho wa

Inaendelea Uk. 7





misingi ya utawala bora. Azimio hili linasisitiza kuwa utawala bora haupimwi kwa uzuri wa sera zilivyoandikwa kwenye makaratasi, bali kwa kiwango ambacho sera hiyo inaboresha maisha ya wananchi wa kawaida.

"Kwanza, tunasisitiza kwamba shughuli za kibunge zinapaswa kuzingatia hali halisi za maisha ya wananchi. Kipimo cha kweli cha utawala bora ni matokeo yake katika maisha ya watu, ili kuhakikisha kuwa wote wanapata fursa sawa. Wito huo unayataka mabunge kuhakikisha kuwa sheria, sera na bajeti zinazoandaliwa zinazingatia taarifa na uhalisia wa maisha.Unapaswa kujumuisha tafiti za kisayansi, takwimu rasmi, taarifa kutoka kwa jamii za maeneo husika, pamoja na uhalisia wa wananchi katika maisha yao ya kila siku." Taarifa hiyo ilieleza

Aidha,azimio hili linasisitiza umuhimu wa wabunge kuwa karibu na wananchi kukutana ana kwa ana na wanaowawakilisha, kuwafikia kwa urahisi na kusikiliza maoni na mahitaji yao. Jambo hili ni muhimu zaidi kwa wananchi wanaoishi maeneo ya mbali, wenye mahitaji maalumu na wanaokabiliwa na hali ngumu, ikiwemo majanga na migogoro.

Zaidi ifahamike kuwa uaminifu si bidhaa inayoweza kutengenezwa kupitia mikakati ya mawasiliano pekee, bali ni jambo linalopatikana kwa kuwa karibu na wananchi na kutekeleza ahadi kwa vitendo. Kwa taasisi hii kubwa ya kimataifa inayowakutanisha wabunge kutoka nchi mbalimbali, huu ni ujumbe kwa taasisi za kidemokrasia zilizopoteza imani ya wananchi wengi wanaowawakilisha.

Mkutano uliazimia kuzingatia uhalisia wa maisha ya wananchi katika msingi wa shughuli za kibunge, kuimarisha uwajibikaji, uwazi na uadilifu kwa taasisi za kibunge, kuimarisha uwazi wa shuguli za kibunge na ushirikishwaji wa wananchi na kuendeleza juhudi za kushughulikia changamoto za muda mrefu za wanachi.

"Hakuna Maamuzi Kuhusu Sisi Bila Ushirikishwaji Wetu": Azimio Kuhusu Haki za Watu Wenye Ulemavu

Azimio kuu la pili la Mkutano wa 153 wa Umoja wa mabunge Duniani (IPU) lilijikita katika haki na ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu, ambao mara nyingi maamuzi yanayowahusu hufanywa bila wao kushirikishwa ipasavyo. Azimio hilo, lililopewa jina la Maendeleo Jumuishi ya Kijamii kwa Wote: Mikakati ya Kibunge ya Kukuza Haki na Uwezeshaji wa Watu Wenye Ulemavu, linaeleza kuwa ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu ni suala la haki za binadamu, uwakilishi wa kidemokrasia na maendeleo endelevu, badala ya kuwa suala la kuwasaidia kwa huruma pekee.



Kwa muda mrefu, sera kuhusu watu wenye ulemavu zimejikita zaidi katika kuwapatia huduma na msaada. Hata hivyo, Azimio la Arusha linatetea mtazamo unaotambua haki yao ya kushiriki kikamilifu katika maisha ya kijamii na kisiasa, wakiwemo kama wapiga kura, wananchi na watunga sheria.Azimio hili linazitaka serikali kuoanisha sheria za nchi na Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watu wenye Ulemavu, kutenga bajeti maalumu kwa ajili ya utekelezaji wa haki hizo na kuhakikisha watu wenye ulemavu wanashiriki moja kwa moja katika michakato ya kufanya maamuzi.

Msingi wa azimio hili ni kauli inayotumiwa na harakati za kimataifa za kutetea haki za watu wenye ulemavu: "Hakuna maamuzi kuhusu sisi bila sisi."Kwa kuunganishwa na Azimio la Utawala Bora linaosisitiza kuwafikia wananchi wa maeneo ya mbali na makundi yaliyotengwa, Azimio hili linasisitiza ujumbe kwamba demokrasia jumuishi inahitaji taasisi zinazowakilisha wananchi wote, bila kumuacha mtu yeyote nje ya maamuzi yanayohusu maisha yake.

Aidha, linasisitiza kuwa watu wenye ulemavu wenyewe wanapaswa kushiriki katika vyombo na mikutano ambako maamuzi yanayowahusu hufanywa.Taasisi za uwakilishi wa wananchi hupata uhalali wake pale zinapowawakilisha watu wote, wakiwemo wale ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakiachwa nje ya michakato ya maamuzi.

Maafa ya Nepal: Wito wa Msaada Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Kwa mara ya kwanza, Nepal iliwasilisha hoja ya dharura katika Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Ujumbe wa nchi hiyo uliiomba Mkutano Mkuu kuchukua hatua kuhusu mafuriko makubwa ya ghafla na maporomoko ya ardhi yaliyotokea nchini humo mwezi Agosti 2026, na kusababisha maelfu ya watu kufariki au kukosa makazi. Hoja hiyo iliwasilishwa na Dol Prasad Aryal, Spika wa Baraza la Wawakilishi la Nepal.

Hoja hiyo ilikabiliwa na ushindani mkubwa. Kwa mujibu wa kanuni za IPU, ni hoja moja tu ya dharura inayoweza kupitishwa katika kila mkutano. Hoja ya Nepal ilishindana na hoja zilizowasilishwa na Bahrain na Iran. Hata hivyo, ilipata theluthi mbili ya kura zilizohitajika, ikiwa na kura 901 za kuunga mkono, 78 za kupinga na wajumbe 140 walioamua kutopiga kura upande wowote.

Matokeo haya yalionesha kuwa Mkutano Mkuu umeamua kuipa kipaumbele changamoto ya majanga yanayohusiana na mabadiliko ya tabianchi na matatizo yanayoikabili milima katika maeneo mbalimbali duniani.



Azimio lililopitishwa halikuishia tu kuonesha wasiwasi kuhusu majanga hayo, bali lilipendekeza hatua za vitendo za kusaidia nchi kujiandaa na kukabiliana nayo. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha mifumo ya tahadhari ya mapema inayovuka mipaka ya nchi, ili wananchi waweze kupata taarifa za hatari kabla mafuriko hayajafika katika maeneo yao.

Azimio hilo pia linazitaka nchi zilizo katika hatari kubwa kupata teknolojia za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ambazo nyingi haziwezi kumudu gharama zake. Aidha, linazitaka Bunge kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa ahadi za Serikali kuhusu tabianchi na kuhakikisha kuwa ahadi zinazotolewa katika

mikutano ya kimataifa zinatekelezwa kwa vitendo.

Azimio hilo pia linaangazia umuhimu wa kulinda barafu za milimani, ambazo ni chanzo muhimu cha maji kwa mamilioni ya watu barani Asia. Barafu hizo zinapoendelea kuyeyuka, upatikanaji wa maji kwa jamii zinazoishi maeneo ya chini ya milima unakuwa hatarini. Azimio linataka msaada wa kifedha na kitaalamu kuwafikia wananchi wanaoathiriwa zaidi na majanga ya tabianchi, hasa wale ambao wamechangia kwa kiwango kidogo zaidi kusababisha mabadiliko hayo.

Ujumbe mkuu wa azimio hili ni haki katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Nchi



“Kuimarisha Utawala Bora na Kuiwezesha Jamii kupitia Ushirikishwaji, Imani na Fursa kwa Wote”

zinapaswa kugawana wajibu, kuhakikisha serikali zinawajibika na kushirikiana kusaidia jamii zinazokabiliwa na hatari kubwa zaidi.
Katika Mkutano wa Arusha, Nepal ilionesha kuwa hata nchi ndogo inaweza kuathiri ajenda ya kimataifa inapowasilisha hoja yenye uzito na ushawishi.

Katika dunia ambayo ushawishi mara nyingi huhusishwa na nguvu za kiuchumi na kijeshi, mafanikio ya Nepal yalionesha kuwa mateso ya wananchi wake na uzito wa ujumbe wake vinaweza pia kuvuta hisia za dunia na kuifanya jumuiya ya kimataifa kuzingatia suala muhimu.

AI na Mustakabali wa Ajira

Kamati ya Kudumu ya Maendeleo Endelevu ya IPU inatambua kuwa akili mnemba (AI) inabadilisha soko la ajira, ikileta fursa mpya na changamoto kwa haki za wafanyakazi, ujuzi na

usawa wa kiuchumi. Katika tamko la kamati yakudumua ya Maendeleo Endelevu imesisitiza umuhimu wa sera zitakazohakikisha teknolojia hii inawanufaisha watu wote na kuchangia maendeleo jumuishi na endelevu.

Pamoja na changamoto hizo, AI inaweza kuongeza uzalishaji, kuchochea ubunifu na ujasiriamali, kuboresha huduma za umma na kuunda fursa mpya za ajira. Hata hivyo, manufaa haya yanaweza yasigawanywe kwa usawa, hasa katika nchi zenye upungufu wa miundombinu ya kidijitali, mitaji, teknolojia na wataalamu wenye ujuzi unaohitajika.

Tamko la kamati limebainisha kuwa athari za AI katika ajira bado zinaendelea, na matokeo yanatofautiana kati ya nchi na sekta. Kwa sasa, ushahidi haujaonesha upotevu mkubwa wa ajira kwa kiwango kikubwa, ingawa taarifa kutoka sekta isiyo rasmi na maeneo mengi ya dunia bado ni chache. Hata hivyo, mabadiliko makubwa yanatarajiwa katika miaka ijayo, yakiathiri makundi mbalimbali kwa namna tofauti, "Vijana Mahitaji ya ajira yanaweza kubadilika, lakini ujuzi wa kidijitali na AI unaweza kuwasaidia kupata fursa mpya, Wanawake Wanaweza kuathirika zaidi kutokana na wengi wao kufanya kazi za ukarani na utawala.

Hivyo, sera zinapaswa kuhakikisha wanapata fursa sawa katika ajira zinazotokana na matumizi ya AI, Nchi zinazoendelea: Mabadiliko ya kiteknolojia yanaweza kuathiri njia za kukuza uchumi, huku wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi wakikosa hifadhi ya jamii. Upungufu wa miundombinu, ujuzi na mitaji unaweza pia kuzuia biashara ndogo na za kati kunufaika na AI." Taarifa hiyo ilieleza

Aidha kwa mujibu wa azimio hilo athari za AI zitategemea kwa kiasi kikubwa maamuzi ya sera za umma. Kwa kutumia mamlaka yao ya kutunga sheria, kusimamia serikali na kuchunguza bajeti, mabunge yana wajibu wa kuhakikisha matumizi ya AI yanaheshimu haki za wafanyakazi, yanaongeza uwezo wa binadamu na kuboresha ubora wa kazi bila kuondoa uwajibikaji na usimamizi wa kibinadamu.

Pia, inasisitiza umuhimu wa mashauriano kati ya serikali, waajiri na wafanyakazi. Mafunzo endelevu, kuongeza ujuzi na elimu kuhusu matumizi ya AI yanapaswa kupewa kipaumbele ili kuwawezesha wafanyakazi, hasa vijana, kukabiliana na mabadiliko ya kiteknolojia.

Kwa kuzingatia mabadiliko yanayosababishwa na akili mnemba (AI) katika soko la ajira, Kamati imependekeza kuwa Bunge Wanachama wa IPU kuchukua hatua zifuatazo: Kuimarisha sheria na sera za AI na ajira ili kuhakikisha zinatambua athari za teknolojia hiyo, kulinda haki za wafanyakazi na kukuza maendeleo ya kiuchumi jumuishi na endelevu, Kuwekeza katika elimu na ujuzi kupitia usimamizi wa serikali na bajeti, kuimarisha mafunzo ya maisha yote, kuweka njia za kuwawezesha vijana kuingia katika soko la ajira na kutoa hifadhi ya jamii kwa wafanyakazi wanaoathiriwa na mabadiliko hayo, Kuhakikisha ufuatiliaji wa athari za AI kwa kuzingatia aina za kazi, umri na jinsia, ikiwemo katika sekta isiyo rasmi, ili kusaidia maamuzi ya kibunge na kupunguza tofauti za upatikanaji wa fursa.

Kuboresha upatikanaji wa teknolojia na miundombinu ya kidijitali, hasa katika nchi zinazoendelea na jamii ambazo hazijafikiwa vya kutosha na huduma hizo, pamoja na kusaidia biashara ndogo na za kati kutumia AI, Kuimarisha ushirikiano wa kimataifa kwa kubadilishana uzoefu kupitia IPU, Shirika la Kazi Duniani (ILO) na mfumo wa Umoja wa Mataifa, ili kuhakikisha manufaa ya AI yanafika katika nchi zote, ikiwemo nchi za Kusini mwa Dunia, na teknolojia hiyo inatumika kwa uwajibikaji kusaidia maendeleo endelevu na matumizi bora ya rasilimali.



Kulinda Haki za Kibinadamu za Wabunge

Mbali na vikao vikuu vya Mkutano, Kamati ya IPU ya Haki za Binadamu za Wabunge iliendelea na kazi yake ya kulinda wabunge ambao haki zao ziko hatarini. Kamati ilipitia kesi zinazohusu wabunge kutoka Argentina, Colombia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Eritrea, Myanmar, Tunisia na Türkiye, na kufanya maamuzi kuhusu kesi hizo.



Kamati hupokea na kuchunguza malalamiko kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu dhidi ya wabunge, yakiwemo vitisho, kukamatwa, kufunguliwa mashtaka isivyo haki, kuzuiwa kutekeleza majukumu yao na kunyang'anywa nyadhifa zao za kibunge. Hukusanya taarifa kutoka kwa wahusika mbalimbali, kutathmini kesi na kuwasiliana na mamlaka za nchi husika ili kutafuta suluhu. Pia, inaweza kutoa mapendekezo na kutaka hatua zichukuliwe kulinda haki za wabunge walioathirika.

Kupitia mchakato huu, Kamati inalenga kuhakikisha kuwa wawakilishi waliochaguliwa na wananchi wanatekeleza majukumu yao bila vitisho, mateso au vikwazo visivyo vya haki. Kazi yake ni muhimu kwa sababu ukiukwaji wa haki za wabunge unaweza pia kudhoofisha haki za wananchi wanaowawakilisha na kudhoofisha taasisi za kidemokrasia.

Shughuli za Kamati zinaonesha hatari zinazowakabili baadhi ya wawakilishi waliochaguliwa na wananchi, pamoja na umuhimu wa ushirikiano wa mabunge kimataifa. Kwa kuchunguza kesi na kushirikiana na mamlaka husika, IPU hutoa jukwaa la kutetea haki za wabunge na kuhimiza uwajibikaji, haki na demokrasia.

"Kwa msingi, kulinda wabunge ni zaidi ya kulinda watu binafsi; ni kulinda haki ya wananchi ya kuwakilishwa." Viongozi waliochaguliwa wanaponyamazishwa, kutishiwa au kuzuiliwa isivyo haki, demokrasia yenyewe hudhoofika. Kwa kushikamana bila kujali mipaka ya nchi, mabunge yanaweza kuhakikisha kuwa hakuna mwakilishi anayeachwa peke yake anapokabiliwa na vitendo vya ukandamizaji, na kwamba sauti za wananchi anaowahudumia hazinyamazishwi.

Mafanikio ya Kihistoria

Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) uliofanyika Arusha uliweka historia kwa kuweka rekodi ya kiwango cha juu zaidi cha ushiriki wa wanawake katika mikutano ya umoja huo katika kipindi cha miaka 137 tangu kuanzishwa kwake. Idadi ya wanawake ilifikia asilimia 39.4 ya wabunge wote waliohudhuria mkutano huo, hatua inayodhihirisha maendeleo katika kukuza ushiriki wa wanawake katika uongozi na maamuzi ya kisiasa.

Mafanikio haya yana uzito wa kipekee ikizingatiwa kuwa IPU ilipoanzishwa mwaka 1889, wanawake walikuwa na nafasi chache sana za kisiasa, huku ni nchi chache tu zilizowaruhusu kupiga kura. Kufikia kiwango ambacho wanawake wanakaribia wawili kati ya kila washiriki watano si mafanikio ya kitakwimu pekee, bali pia ni hatua muhimu katika kuimarisha demokrasia. Ushiriki wao huongeza mitazamo mbalimbali katika mijadala, husaidia kuibua masuala yanayoathiri jamii na kuhakikisha kuwa uzoefu na mahitaji ya wanawake yanazingatiwa katika mchakato wa kufanya maamuzi. Kwa msingi huo, ongezeko la ushiriki wa wanawake lilikuwa miongoni mwa mafanikio muhimu zaidi ya Mkutano wa 153 Jijini Arusha.

Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) uliofanyika Arusha ulikuwa fursa muhimu ya kuimarisha mazungumzo na ushirikiano kati ya nchi, hususani zile zinazokabiliwa na migogoro. Kupitia mkutano huo, wajumbe kutoka nchi kadhaa zilizo katika migogoro waliweza kukutana katika jukwaa lisiloegemea upande wowote, licha ya kuwepo kwa changamoto katika mahusiano ya kidiplomasia kati ya serikali zao.

Katika mazingira ambayo serikali zinazohusika katika vita mara nyingi hushindwa au hukataa kuzungumza moja kwa moja, diplomasia ya kibunge hutoa fursa kwa wawakilishi waliochaguliwa na wananchi kukutana, kubadilishana mawazo na kudumisha mawasiliano. Hii ni fursa muhimu ya kujenga

uelewano na kuzuia mawasiliano kati ya pande zinazokinzana kukatika kabisa.

Kwa msingi huo, diplomasia ya kibunge ina nafasi muhimu katika juhudi za kujenga amani, hasa pale mazungumzo rasmi kati ya serikali yanapokwama. Uwezo wake wa kufungua njia za mazungumzo na kuendeleza uhusiano kati ya pande zinazokinzana ni mojawapo ya mchango muhimu wa mabunge katika kukuza amani duniani.

SPIKA ZUNGU: MAAZIMIO YA MKUTANO WA 153 WA IPU YASIBAKI KWENYE MAKARATASI

Na Lawrence Raphaely

Spika wa Bunge la Tanzania na Rais wa Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu amewaasa Wajumbe kuhakikisha kuwa maazimio ya mkutano huo hayabaki kuwa maneno tu kwenye karatasi, badala yake wayapeleke katika mabunge yao ya kitaifa na kuyageuza kuwa sheria, sera na hatua madhubuti zinazoboresha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Zungu aliyasema hayo wakati akitoa hotuba ya kufunga Mkutano wa 153 wa IPU tarehe 9 Oktoba, 2026 katika Ukumbi wa Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC) Jijini Arusha.

"Kama nilivyosema wakati wa ufunguzi wa mkutano huu, tunawakilisha nchi, mifumo ya kisiasa, tamaduni na mitazamo tofauti. Hata hivyo, tunashiriki jukumu moja la pamoja la kuwahudumia wananchi wetu na kuchangia katika kuleta dunia yenye amani zaidi, haki na maendeleo endelevu," alisema.

Aliwaasa Wajumbe wa Mkutano huo kuondoka Arusha wakiwa na dhamira mpya ya mazungumzo badala ya migawanyiko, ushirikiano badala ya migongano na ushirikishwaji badala ya kutengana katika makundi.

"Nguvu ya IPU inatokana na uwezo wetu wa kuungana licha ya tofauti zetu. Mikutano ya kimataifa lazima itusaidie kuielekeza dunia katika njia mpya, inayozingatia mazungumzo, utu, heshima, ushirikishwaji na mshikamano," alisema.

Kwa upande mwingine Mhe. Zungu alimpongeza Rais Mteule wa IPU, Mhe. Milton Dick, Spika wa Bunge la Wawakilishi la Australia aliyechaguliwa wakati wa Mkutano huo.

Mheshimiwa Dick anachukua nafasi ya Spika Mstaafu wa Bunge la Tanzania, Mhe. Dkt. Tulia Ackson ambaye anamaliza muda wake.

Mheshimiwa Zungu alimshukuru pia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kuandaa mkutano huo nchini.

Mheshimiwa Zungu aliwashukuru pia Watanzania wote hususan wakazi wa Arusha kwa kuwakaribisha wajumbe wote kwa uchangamfu na urafiki.

"Dunia imeshuhudia kuwa Tanzania ni nchi ya amani, umoja na ukarimu. Kwa kila mtu aliyefanya kazi nyuma ya pazia kufanikisha Mkutano huu, tunawashukuru," alisisitiza.



Dkt. Samia Ahimiza Usimamzi wa Rasilimali za Umma katika Mkutano wa IPU

Na Lawrence Raphaely

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameyataka mabunge kuimarisha usimamizi wa rasilimali za umma na uwajibikaji wa Serikali, akisisitiza kuwa wananchi wanatarajia wawakilishi wao kulinda maslahi yao na kuhakikisha mahitaji yao yanazingatiwa katika maamuzi.

Rais Dkt. Samia alitoa ujumbe huo kupitia picha mjongeo iliyooneshwa katika ufunguzi wa Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Jumatatu, Oktoba 5, 2026 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC).





Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba, alimwakilisha Rais Dkt. Samia katika ufunguzi rasmi wa mkutano huo uliofanyika Oktoba 5 hadi 9, 2026.

Alisema mamlaka ya mabunge yanatokana na wananchi, hivyo yana wajibu wa kutunga sheria kwa maslahi ya umma, kuchunguza mgawanyo na matumizi ya rasilimali na kuziwajibisha Serikali. Ameeleza kuwa Serikali yake inaheshimu jukumu la Bunge la kuisimamia na kuishauri kwa kuwa linaimarisha utendaji na uwajibikaji kwa Watanzania.

Rais Dkt. Samia alisema kaulimbiu ya mkutano kuhusu kuimarisha utawala bora na kuziwezesha jamii kupitia ushirikishwaji, kuaminiana na fursa kwa wote inaendana na changamoto za sasa duniani. Amehimiza mabunge kutathmini makubaliano yanayofikiwa na Serikali na kuendeleza ushirikiano unaovuka tofauti za kisiasa na mipaka ya nchi.

Kwa upande wake Waziri Mkuu akizungumza katika ufunguzi huo, alisema mabunge yana nafasi muhimu katika kuhakikisha taasisi za umma zinaitikia mahitaji ya wananchi kupitia utungaji wa sheria, uidhinishaji wa matumizi ya fedha na usimamizi wa shughuli za Serikali.

Ametaja kuimarishwa kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), iliyotengewa zaidi ya shilingi bilioni 132 katika mwaka wa fedha 2026/2027, kuwa sehemu ya juhudi za kuimarisha usimamizi wa rasilimali za umma.

Dkt. Mwigulu alisema Rais Dkt. Samia anaamini katika utawala wa kikatiba na mgawanyo wa madaraka, akisisitiza kuwa taasisi imara na huru ni muhimu katika kujenga jamii zenye ustawi, utulivu na ushirikishwaji.

Alisema changamoto za mabadiliko ya tabianchi, dharura za afya, misukosuko ya kiuchumi na maendeleo ya teknolojia zinahitaji majadiliano, ushirikiano na diplomasia ya kibunge.

Alisisitiza kuwa utawala bora unahusu kulinda utu wa binadamu, kuhakikisha kila mwananchi anasikilizwa, jamii zinawezeshwa na kila kizazi kinapata fursa ya kustawi.

Aidha, ametaja maendeleo katika sekta za nishati, reli, elimu na afya kuwa miongoni mwa hatua za kuboresha maisha ya wananchi chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia.

Pia, alimpongeza Rais wa IPU, Dkt. Tulia Ackson, kwa uongozi wake katika taasisi hiyo, akisema ameiletea Tanzania heshima na kuonesha umuhimu wa fursa sawa katika uongozi wa kimataifa.

Awali, akizungumza wakati wa ufunguzi huo, aliyekuwa Rais wa IPU, Dkt. Tulia Ackson alisema Mabunge yanapaswa kuhakikisha rasilimali za umma zinawafikia wanaozihitaji na kupima mafanikio ya sera kwa matokeo yake katika maisha ya wananchi. Amehimiza ushiriki wa wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na makundi yanayotengwa katika maamuzi ya umma.

"Mti mmoja haujengi msitu," amesema, akisisitiza umuhimu wa mshikamano na ushirikiano katika kukabiliana na changamoto za dunia. Ameeleza kuwa hiyo ni hotuba yake ya mwisho ya ufunguzi wa Mkutano wa IPU akiwa Rais wa Taasisi hiyo, baada ya kuhudumu kwa miaka mitatu.

Katika ujumbe uliowasilishwa kupitia picha mjongeo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa aliyataka mabunge kuimarisha uwajibikaji, ushirikishwaji na kuaminiana kati ya wananchi na taasisi za umma. Naye mwakilishi wa Umoja wa Mataifa nchini alisisitiza kuwa ahadi za maendeleo zinahitaji kuungwa mkono na bajeti, sheria na usimamizi wa utekelezaji.

Katibu Mkuu wa IPU, Balozi Anda Filip, aliyataka mabunge kuipa kipaumbele mijadala kuhusu akili unde (AI), akisisitiza usimamizi wa kidemokrasia na ushirikiano wa kimataifa ili kuhakikisha teknolojia hiyo inatumika kwa usalama na kuendelea kuwa chini ya udhibiti wa binadamu.

Spika Zungu Asisitiza Dunia Kushirikiana wakati Akihutubia Ufunguzi wa Mkutano wa 153 wa IPU

Na Debora Sanja

Spika wa Bunge la Tanzania, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu ametoa rai ya Mataifa kuungana katika kutatua changamoto zinazojitokeza kwa kuwa hakuna upande unaoweza kufanikiwa bila upande mwingine.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Jumatatu, Oktoba 5, 2026, katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC) Mheshimiwa Spika amesema kupitia mabunge, tofauti zinaweza kubadilishwa kwa mazungumzo na maslahi yanayopingana yanapatanishwa kupitia hoja.

"Sisi ni mahali ambapo tofauti zinabadilishwa kwa mazungumzo, maslahi yanayopingana yanapatanishwa kupitia hoja na utu wa kila binadamu unalindwa,hatushughulikii kesho tofauti.

"Tuna ubinadamu mmoja na hatima ya pamoja. Hatuna tatizo la Kusini mwa Dunia au tatizo la Kaskazini mwa Dunia. Tuna tatizo la kibinadamu. Na linahitaji suluhisho la kibinadamu. Kaskazini ina teknolojia na mtaji, Kusini ina rasilimali, vijana, na ustahimilivu. Hakuna upande unaoweza kufanikiwa bila mwingine," alisema.

Alisema dunia ya kesho inahitaji lugha ya ushirikiano na ubunifu badala ya lugha ya utegemezi na hisani chini ya chombo kimoja cha kibunge.

"Hakuna dunia mbili ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea, kwa miongo mingi msamiati wetu wa kimataifa umeundwa na maneno kama vile wafadhili na wapokeaji, walioendelea na wanaoendelea, misaada na usaidizi.

"Lugha kama hii inaweza kuelezea vipengele vya historia yetu, lakini haielezei ipasavyo dunia tunayoingia. Dunia inahitaji madini muhimu na madini adimu kutengeneza betri, teknolojia za nishati mbadala, magari ya umeme, vifaa vya elektroniki vya hali ya juu na teknolojia nyingine muhimu kwa mustakabali wa uchumi wetu.

"Sisi si dunia mbili, sisi ni dunia moja inayojaribu kujenga mustakabali mmoja kwa wanadamu. Madini adimu yaliyo chini ya Afrika na Amerika ya Kusini yanaweza kuendesha mustakabali wa kijani unaobuniwa Ulaya na Amerika. Vijana wa Kusini wanaweza kuendesha uchumi wa Kaskazini," alisisitiza.

Alisema mustakabali wa dunia haupaswi kuwa mustakabali ambapo Kusini inatoa rasilimali wakati Kaskazini inanasa sehemu kubwa ya maarifa, teknolojia na thamani na kwamba jibu si kufunga milango kwa uwekezaji na ushirikiano wa kimataifa.



"Jibu ni ushirikiano ili uwekezaji ulete mtaji na teknolojia, elimu ilete ujuzi, ushiriki wa ndani ulete ajira na ubunifu ulete thamani.

"Tunapokutana hapa kwa Mkutano wa 153, nawahimiza sote Kaskazini mwa Dunia na Kusini mwa Dunia tufanye kazi pamoja kwa ajili ya ubinadamu mmoja na hatima ya pamoja. Tuondoke Arusha tukiwa tumechagua ushirikiano badala ya utegemezi, mshikamano badala ya mgawanyiko na ustawi wa pamoja badala ya fursa zisizo sawa," alisema.

Kaulimbiu ya Mkutano huo wa 153 wa IPU ilikuwa ni "Kuimarisha Utawala Bora, Kupitia Ushirikishwaji, Imani na Fursa kwa Wote".

TANZANIA IMEIMARISHA UTAWALA BORA

Akizungumzia masuala ya Utawala Bora, Spika wa Bunge amesema Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) unafanyika wakati Tanzania ikiwa imefanya juhudi kubwa kujenga utawala bora, Imani ya jamii na fursa jumuishi za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika alisema katika kipindi hiki, Tanzania imeshuhudia mageuzi ya kisiasa na maridhiano ambapo Serikali chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan iliendeleza falsafa ya 4R (Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi, na Kujenga Upya).

Alisema falsafa hiyo imetoa kipaumbele kikubwa katika masuala ya haki za binadamu, demokrasia na utawala jumuishi.

"Kufuatia mageuzi haya, Bunge la Tanzania lilipitisha sheria kadhaa za mageuzi ya kisiasa, ikiwemo Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Serikali za Mitaa na Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa. "Sheria hizi zinalenga kuhakikisha michakato ya uchaguzi iliyo huru, yenye uwazi na inayoaminika zaidi," amesema.

Aidha, alieleza kuwa utawala bora unategemea ujumuishi na uwezeshaji, jambo ambalo Bunge la Tanzania limefanikiwa kutekeleza mifumo ya kikatiba na kisheria inayoongeza uwakilishi wa wanawake Bungeni na katika Serikali za Mitaa.

"Sheria ya Vyama vya Siasa sasa inaelekeza wazi ujumuishaji wa makundi ya kijamii (vijana, wanawake na watu wenye ulemavu) ndani ya miundo ya ndani ya vyama na uteuzi wa wagombea.

"Tunajivunia kuwa uwakilishi wa wanawake katika Bunge letu umekuwa ukiongezeka kwa muda hadi kufikia 39.5% kwa sasa," alisema.

DIRA YA TAIFA

Mhe. Spika alisema Dira ya Taifa ya 2050 inatambua utawala bora, amani, usalama na utulivu kama msingi wa maendeleo endelevu. "Juu ya msingi huu ndipo nguzo tatu za Dira zimesimama, uchumi imara, jumuishi na shindani, uwezo wa watu na maendeleo ya jamii na uadilifu wa mazingira na ustahimilivu wa tabianchi.

"Muundo huu unaweka wazi kuwa utawala bora ni kiwezeshaji cha matarajio yetu yote ya maendeleo, " alisema.

Alisema chini ya uongozi wa maono wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Dira ya 2050 si tu hati bali ni mkataba kwamba amebadilisha ndoto ya miaka 25 kuwa ramani inayopimika kutoka uchumi wa dola bilioni 85 hadi uchumi wa dola trilioni 1 huku utawala bora ukiwa ndio msingi wake

> ***"Tunajivunia kuwa uwakilishi wa wanawake katika Bunge letu umekuwa ukiongezeka kwa muda hadi kufikia 39.5% kwa sasa."***



MASPIKA WA GHANA NA ZIMBABWE WAMMWAGIA SIFA DKT. TULIA: "UMEITENDEA HAKI AFRIKA"

Na Deonisius Simba

Maspika wa mabunge barani Afrika walimpongeza aliyekuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Mhe. Dkt. Tulia Ackson, kwa kuongoza chombo hicho kwa weledi mkubwa na kuliwakilisha vyema bara la Afrika katika ulingo wa kimataifa.

Pongezi hizo zilitolewa, tarehe 4 Oktoba, 2026, wakati wa kikao cha Kikundi cha Kijiografia cha Kisiasa cha Afrika (African Geopolitical Group) kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC). Kikao hicho kilikuwa mahsusi kwa ajili ya maandalizi ya ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa 153 wa IPU uliofanyika jijini Arusha tarehe 5 hadi 9 Oktoba, 2026.

Akizungumza katika kikao hicho, Rais wa Kikundi hicho cha Afrika ambaye pia ni Spika wa Bunge la Ghana, Mheshimiwa Alban Bagbin, alibainisha kuwa Dkt. Tulia anaacha alama na taswira nzuri isiyofutika kupitia kiti cha Urais wa IPU.

"Uongozi wa Dkt. Tulia umelipa heshima kubwa bara la Afrika na kutufanya sote tuwe na furaha. Kundi hili litaendelea kumuunga mkono kwa kila hatua," alisema Mhe. Bagbin.

Naye mwanachama wa kikundi hicho ambaye ni Spika wa Bunge la Zimbabwe, Mheshimiwa Jacob Mudenda, aliongeza kuwa Dkt. Tulia alistahili kushika nafasi hiyo kubwa duniani kwa kuwa "ameitendea haki nembo ya Afrika."

Kwa upande wake, Dkt. Tulia, ambaye pia ni Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitumia fursa hiyo kutoa shukrani za dhati kwa viongozi na wabunge wote wa Afrika kwa ushirikiano mkubwa waliompa katika kipindi chote cha miaka mitatu ya uongozi wake juu ya chombo hicho kikubwa cha diplomasia ya kibunge duniani.

Dkt. Tulia aliwaasa wajumbe hao kufanya maamuzi ya busara katika uchaguzi unaokuja ili kupata mrithi atakayeendeleza mapambano ya bara hilo.

"Ni muhimu kumchagua kiongozi mpya ambaye atakuwa na sikio la kuwasikiliza, mnyenyekevu, na mwenye utayari wa kupigania maslahi na vipaumbele vya bara la Afrika kwenye meza ya maamuzi ya dunia," Dkt. Tulia.

SPIKA ZUNGU: TANZANIA IMEPIGA HATUA KUBWA KATIKA UWAWAKILISHI WA WAWANAKE

Na Lawrence Raphaely

Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb) amesema maendeleo yaliyopatikana katika kuongeza uwakilishi wa wanawake mabungeni yanatia moyo.

Aliyasema hayo wakati akifungua Mkutano wa Jukwaa la Wanawake wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) Oktoba 5, 2026 katika Ukumbi wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC).

Alisema kwa upande wa Tanzania, uwakilishi wa wanawake bungeni ni asilimia 39.5,"

Hata hivyo, alisema uwakilishi pekee hautoshi hivyo Mabunge Wanachama wa IPU yanapaswa kuendelea kushughulikia vikwazo vinavyoathiri ushiriki madhubuti, uongozi na ushawishi wa wanawake katika michakato ya kisiasa na kibunge.

"Jukwaa hili linatoa fursa muhimu ya kubadilishana uzoefu na kujadili masuala yanayolenga kuimarisha ushiriki wa wanawake katika maamuzi"



"Tunapokutana hapa Tanzania, hebu tuthibitishe tena kuwa mabunge yanayoshirikisha makundi yote ni mabunge imara zaidi," amesema.

Alisema kuwawezesha wanawake kushiriki kikamilifu na kwa usawa katika nyanja ya kisiasa kunaimarisha taasisi za kidemokrasia na kuchangia katika utawala unaowakilisha vyema wananchi na kujali mahitaji yao.

Aliwahimiza washiriki kutumia Jukwaa hilo kubadilishana uzoefu kwa uwazi, kujenga ushirikiano na kubainisha hatua madhubuti za kuchukua katika mabunge ya nchi wanachama.

"Majadiliano haya yanapaswa kutusaidia kutoka hatua ya ahadi hadi utekelezaji wa vitendo," alisisitiza.

Aliongeza kuwa kuondoa vikwazo vya kimfumo na kuhakikisha wanawake wanapata fursa sawa ya kushiriki katika maamuzi, kunajenga imani katika taasisi na kufungua fursa za pamoja zinazohitajika ili kujenga dunia yenye haki na inayoshirikisha watu wote.

Tuli Aahidi Kuendeleza Ushirikiano Jukwaa la Wanawake IPU

Na Debora Sanja

Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Spika wa Bunge Mstaafu wa Bunge la Tanzania Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson ameahidi kuendelea kusimama na wabunge wa Jukwaa la Wanawake wa Umoja umoja huo katika kusimamia ajenda za wanawake licha ya kumaliza muda wake.

Dkt. Tulia ametoa kauli hiyo wakati akitoa hutoba yake ya mwisho katika Mkutano wa Jukwaa hilo uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa (AICC) jijini Arusha uliofanyika Oktoba, 2026.

Dkt. Tulia amehitimisha kipindi chake cha miaka mitatu cha Rais wa IPU katika Mkutano huu wa 153 uliofanyika jijini Arusha ambapo Rais mpya wa umoja huo alichaguliwa.

Aliwashukuru Ofisi ya Wabunge Wanawake, sekratarieti na wabunge wanawake na wanaume kwa ushirikiano wao wa dhati kwake ambao umempa nguvu ya kutekeleza majukumu yake wakati wote wa kipindi chake.

"Katika Jukwaa langu la kwanza nilisema tunahitaji kufanya vizuri zaidi na kwa kasi zaidi. Bado tunahitaji kufanya hivyo. Wanawake katika ukumbi huu wameleta mabadiliko na tutaendelea kusonga mbele. Daima nitasimama pamoja nanyi," alisema.

"Asanteni kwa heshima ya kuhudumu pamoja nanyi, na kwa wakati huu wa leo," alisema.

Alisema wakati alipochaguliwa kuwa Rais wa IPU, tukio la kwanza alilokutana lilihusu ukatili dhidi ya wanawake mabungeni na alisema kwamba unyanyasaji wa wanawake kwenye siasa haupaswi kukubaliwa au kuchukuliwa kama jambo la kawaida.

"Hili ni suala la haki za binadamu, ni suala la demokrasia. Ninaamini hivyo hivyo kwa nguvu hadi leo,najivunia kuongoza umoja huu ambao unatekeleza kwa vitendo kile unachokihubiri," alisema.

Alisema wakati wa uongozi wake walirekebisha Katiba, Sera na Kanuni ili kuweka usawa wa kijinsia katika IPU kama lengo la umoja huo.

"Sera yetu ya kwanza kabisa ya kupinga unyanyasaji katika Mabunge na matukio ya IPU ilipitishwa. Sera hii inaweka kiwango kiko wazi cha unyanyasaji ikiwemo unyanyasaji wa kingono. Sera hii inamuhusu kila mtu na pia tuna njia zilizo wazi za kuripoti na kushughulikia matukio," alisema.

Akizungumzia mafanikio mengine yaliyopatikana katika kipindi chake ni kuchaguliwa kwa Katibu Mkuu Mwanamke kwa mara ya kwanza Balozi Anda Filip jambo ambalo atajivunia milele.
Aidha, alisema maendeleo ya wanawake hayawezi kupatikana bila kuwashirikisha wanaume hivyo lazima mazungumzo ya pamoja yaendelee hivyo akasisitiza wanaume wengi zaidi waendelee kushirikishwa.

"Usawa pia unamaanisha mamlaka kwa wanawake katika utofauti wetu wote, wanawake vijana, wanawake kutoka jamii zilizotengwa na wanawake wenye ulemavu tayari wanajipanga na kuongoza, mabunge yetu yaende sambamba nao," alisema.

Alisema Rasimu ya Azimia litakalojadiliwa katika Mkutano huu kuhusu haki za watu wenye ulemavu litatoa nafasi ya kufanya dhamira hiyo kuwa ya kweli.

"Wasikilizeni wanawake wenye ulemavu, leteni vipaumbele vyao kwenye meza ya maamuzi, tuweke sawa uwanja kwao ili waweze kugombea uchaguzi, kuingia kwenye kumbi zetu, kuchukua nafasi ya kuzungumza na kufanya maamuzi. Hili limechelewa kwa muda mrefu sasa tuthibitishe kwa vitendo," alisema.

Alisema Jukwaa la Wanawake la IPU ni kama ni mnara wa taa lakini inahitajika dhamira ya kweli ili liendelee kung'aa.

"Asanteni kwa heshima ya kuhudumu pamoja nanyi, na kwa wakati huu wa leo."

Ni Wakati Muhimu wa Kutathimini Jinsi Mabunge Yanavyoweza Kukidhi Matarajio ya Wananchi

Na Debora Sanja

Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu amesema Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) si fursa pekee ya Wabunge kukutana kama wawakilishi wa Mabunge, bali pia ni wakati muhimu wa kutathmini jinsi mabunge yanavyoweza kukidhi matarajio ya wananchi na kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika jamii.

Mheshimiwa Spika aliyasema hayo wakati akihutubia Mkutano Mkuu wa 153 wa IPU mara baada ya kuchaguliwa kuwa Rais wa Mkutano huo Oktoba 6, 2026.

Alisema wawakilishi wa wananchi wana wajibu wa kuhakikisha kuwa ahadi za kitaifa zinatafsiriwa kuwa matokeo yanayoonekana na yenye tija.

"Kupitia utungaji wa sheria, uwakilishi, na usimamizi ni lazima mabunge yaendelee kuwa na uhusiano wa karibu na uhalisia wa maisha ya kila siku ya wananchi tunaowawakilisha," amesema.


Alisema Mkutano huo unafanyika wakati ambapo dunia inakabiliwa na changamoto kubwa ambazo ni pamoja na kupungua kwa imani katika taasisi za umma, ukosefu wa usawa, migogoro na ukosefu wa usalama.

"Watu duniani kote wanadai uwajibikaji zaidi, taasisi zinazojali na kuitikia mahitaji ya wananchi, fursa sawa na ushiriki wenye tija katika maamuzi yanayohusu maisha yao," alisema.

"Mambo haya yanatukumbusha kuwa utawala bora si suala la taasisi na mifumo pekee bali ni suala linalowahusu watu," alisisitiza.
Ameongeza kwamba changamoto zilizopo ni mtambuka kiasi kwamba hakuna Bunge, Serikali au taasisi yoyote inayoweza kuzitatua peke yake.

"Mabadiliko ya tabianchi, mabadiliko ya kiteknolojia, ukosefu wa usawa, shinikizo la kiuchumi, migogoro na matarajio yanayobadilika ya wananchi wetu yanahitaji ushirikiano mkubwa na hatua za pamoja," alisema.

Kufutia changamoto hizo, Spika Zungu alitoa



wito kwa Mabunge Duniani kutunga sheria zinazolinda haki za watu hasa wale ambao mara nyingi sauti zao hazisikiki.

"Ili kubadilisha uhusiano kati ya nchi za Kaskazini na Kusini mwa dunia ni lazima tuvuke hatua ya matamko tu na kugeuza malengo yetu kuwa mifumo madhubuti ya utekelezaji," alisema.

Alisema matarajio yake ni kwamba Mkutano wa 153 wa IPU utatoa matokeo ya kivitendo yanayoweza kutekelezeka na yenye mtazamo wa mbele.

"Tunaamini kujifunza kutokana na uzoefu wa mabunge mengine, kubadilishana mbinu zilizofanikiwa katika nchi zetu na kubaini masuluhisho yanayoweza kutumika katika mazingira tofauti," amesema.

"Hivyo basi, Mkutano huu uwe jukwaa la kurejesha imani, kuimarisha uwajibikaji, kuwawezesha wananchi na kuleta fursa kwa wote," amesisitiza.



"Tanzania imejenga jina kubwa sana katika d
sana Mheshimiwa Rais, lakini pamoja na nchi,
wake, kwa kushirikiana na Serikali na Bunge la J
wa Tanzania katika maandalizi ya mkutano huu.

MHE. ZUNGU: TANZANIA IMEWEKA HISTORIA KATIKA MKUTANO WA 153 WA IPU

Na Lawrence Raphaely

Spika wa Bunge, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu amesema Tanzania imeweka historia Kimataifa katika Mkutano Mkuu wa mwaka wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) kuendeshwa na viongozi wawili wa Tanzania.

Mheshimiwa Zungu aliyasema hayo wakati akizungumza na Waandishi wa Habari wakati wa Mkutano Mkuu wa 153 wa IPU unaofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), Oktoba 6, 2026.



dunia. Tunampongeza , Tanzania na viongozi Jamhuri ya Muungano u." Spika Zungu

Spika wa Bunge la Tanzania alichaguliwa kuwa Rais wa Mkutano Mkuu wa 153 wa IPU kipindi ambacho Rais wa Umoja alikuwa Spika Mstaafu wa Bunge la Tanzania, Mhe. Dkt. Tulia Ackson.

"Kwa mara ya kwanza katika historia ya Bunge hili ambalo lilianzishwa mwaka 1889, linaendeshwa na Watanzania wawili; Rais wa IPU, Dkt. Tulia na Spika wa Bunge la Tanzania. Hii ni historia kwa Tanzania," alisema.

Aidha, alisema historia hiyo itaendelea kuwekwa katika kumbukumbu za Tanzania, akimtaja Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwa sehemu muhimu ya hatua hiyo kwa kuifikisha Tanzania katika nafasi ambayo dunia sasa inaitambua.

Akimzungumzia Spika wa Bunge la Uingereza Sir Lindsay Hoyle ambaye ndiye aliyempendekeza achaguliwe kuwa Rais wa IPU, amesema ushiriki wa Spika huyo katika Mkutano wa 153 wa IPU ni jambo la kihistoria. "Jambo lingine kubwa la kihistoria ni ushiriki wa Spika wa Bunge la Uingereza, Westminster House of Commons katika Mkutano wa 153 wa IPU unaoendelea jijini Arusha.

"Katika kipindi cha zaidi ya miaka 40, Spika wa Bunge la Uingereza, hajawahi kuhudhuria kikao kamili cha IPU. Amekuja nchini Tanzania, jambo hili ni historia kubwa na somo kwa dunia kuhusu hatua ambayo Taifa letu limepiga," alisema.

Alisema kuteuliwa na kupendekezwa kwa Tanzania kuendesha Mkutano huo na Spika wa Bunge la Uingereza, ni ishara ya diplomasia kubwa kwa Tanzania katika medani ya kimataifa.

"Kupendekezwa na Spika wa Uingereza kuwa Rais wa Mkutano huu ni suala la diplomasia kubwa sana duniani. Hii inajenga uhusiano mkubwa kati ya Tanzania, mabunge na mataifa mbalimbali," alisema.

Alisema fursa ya Tanzania kuandaa mkutano huo, inapaswa kutumiwa kujenga uhusiano na ushirikiano zaidi kati ya Tanzania na mabunge



ya mataifa mbalimbali duniani.

Kutokana na mafanikio hayo, Spika Zungu, amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa afya na nguvu alizonazo za kuendelea kuliongoza Taifa, pamoja na juhudi zake katika maandalizi ya mkutano huo nchini Tanzania.
Alisema wajumbe wote waliokuja Tanzania walipokelewa vizuri, huku Tanzania ikionesha uwezo mkubwa wa kushirikiana na mataifa na mabunge mbalimbali duniani.

"Tanzania imejenga jina kubwa sana katika dunia. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, lakini pamoja na nchi, Tanzania na viongozi wake, kwa kushirikiana na Serikali na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika maandalizi ya mkutano huu," alisema.

DIPLOMASIA YA UTALII: WASHIRIKI WA MKUTANO WA IPU WAMWAGIA SIFA HIFADHI YA NGORONGORO

Na Pius Myanda

Wajumbe na washiriki wa Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), walitembelea Hifadhi ya Ngorongoro na Makumbusho ya Urithi wa Kijiolojia (Geopark) yaliyopo Karatu mkoani Arusha.

Wajumbe hao walitembelea maeneo hayo wakati wa Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani uliofanyika katika Ukumbi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC) Oktoba 5 hadi 9, 2026.

Wajumbe waliotembelea hifadhi hizo ni pamoja na Makatibu wa Mabunge, Maspika



na Maafisa Waandamizi kutoka mataifa mbalimbali na kushuhudia upekee wa ikolojia ya Tanzania pamoja na msongamano mkubwa wa wanyamapori, wakiwemo simba, tembo, nyati na mnyama adimu kama faru mweusi.

Akizungumzia umuhimu wa tukio hilo, Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndg. Baraka Leonard, alieleza kuwa ziara hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa vitendo wa diplomasia ya uchumi na utalii.

"Tanzania imebarikiwa kuwa na urithi wa kipekee duniani. Kupitia ujio wa viongozi hawa wa mabunge, hatuishii tu kujadili utawala bora, sheria na demokrasia bungeni, bali tunawapa fursa ya kujionea wenyewe fahari ya nchi yetu. "Tunaamini ushuhuda watakaorudi nao katika nchi zao utakuwa chachu kubwa ya kuitangaza Tanzania na kuwavutia wao wenyewe na familia zao kurejea tena kama watalii," alisema Ndg. Baraka Leonard.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dkt. Hassan Abbasi, alitaja mikakati thabiti iliyowekwa na Serikali katika kuhakikisha wageni hao wanapata uzoefu wa kipekee na usio saulika nchini.

Mkutano huu wa 153 wa IPU, uliwakutanisha washiriki zaidi ya 2000 kutoka mataifa zaidi 150 duniani kote.



KATIBU BARAKA: BUNGE LA TANZANIA LIPO TAYARI KUSHIRIKIANA NA MABUNGE MENGINE

Na Pius Myanda

Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndugu Baraka Leonard, amesema Bunge la Tanzania lipo tayari kujifunza na kushirikishana uzoefu kutoka mabunge mengine duniani.

Katibu wa Bunge alieleza hayo Oktoba 7, 2026 wakati akitoa hotuba katika Mkutano wa Makatibu wa Bunge wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Makatibu hao walikuwa wakishiriki katika Mkutano wa 153 wa IPU uliofanyika jijini Arusha katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC).



"Tunatambua kuwa hakuna Bunge linalojua kila kitu, mbinu yetu ni kujifunza kutoka kwa wengine na kushirikishana uzoefu," amesema. Akizungumza mifumo mbalimbali ya kibunge, alisema hakuna mfumo mmoja ulio bora zaidi ya mwingine na kwamba tofauti ya mifumo hiyo ya kibunge ndiyo inayofanya Umoja huo wa Makatibu wa Bunge kuwa muhimu.

"Tunapotazama mifumo tofauti ya kibunge iliyopo hapa, tunakumbushwa kuwa hakuna mfumo mmoja ulio bora zaidi. Wengine mna mfumo wa mabunge mawili, wengine kama Tanzania tuna Bunge moja.Tofauti hii ndiyo inayofanya umoja huu kuwa muhimu sana.

"Tunakutana si kupanga ni mfumo gani bora zaidi, bali kuelewa ni nini kinachofanya kazi, kwa nini kinafanya kazi na ni mafunzo gani tunaweza kuyachukua," alisema Katibu wa Bunge.

Alisema Umoja wa Makatibu wa Bunge unatoa fursa ya kipekee ya kujifunza kutoka kwa kila Bunge kuhusu taratibu za kibunge, jinsi taasisi za kibunge zinavyohifadhi mwendelezo, kusaidia Wabunge, kukabiliana na mabadiliko na kubaki na ufanisi katika mazingira yanayobadilika kwa kasi.

Akizungumzia kuhusu mabadiliko kwenye Mabunge amesema, Bunge la Tanzania linafanyia kazi mazingira ya mabadiliko ya haraka ikiwemo mabadiliko katika ya matarajio ya wananchi, mabadiliko ya kiteknolojia na kuogeza uwazi.

"Bunge la Tanzania limeingia katika mfumo wa kidijitali kupitia mfumo wa Bunge Mtandao (e-Parliament), ambao unawawezesha Wabunge kupata nyaraka kwa njia ya mtandao na kufanya kazi bila karatasi.

"Pia tumeongeza upatikanaji wa shughuli za Bunge kwa umma. Vikao vya Bunge hurushwa kupitia Televisheni ya Bunge na mitandao ya kijamii. Bunge letu lipo wazi kwa wananchi wanaotaka kufuatilia shughuli moja kwa moja, hasa wanafunzi," amesema.



Katibu wa Bunge aliwakaribisha wageni wote Arusha ambao ni washirika katika usimamizi wa shughuli za kibunge.

"Mimi na timu yangu tumeandaa kila kitu kuhakikisha mkutano huu unatoa mazingira muafaka ya kubadilishana uzoefu, kujifunza na kushirikiana kitaalamu.

"Arusha kwa muda mrefu imehusishwa na diplomasia, majadiliano, ushirikiano wa kikanda na ushiriki wa kimataifa, Mkutano huu pia unakuja katika wakati muhimu sana katika historia ya taasisi za kibunge nchini Tanzania," amesema.

SPIKA ZUNGU: TANZANIA TAYARI KUCHANGIA UZOEFU HUDUMA ZA MAMA NA MTOTO

Na. Debora Sanja

SPIKA wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mussa Azzan Zungu amesema Tanzania ipo tayari kuchangia uzoefu wake katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za mama na mtoto mchanga, afya ya uzazi, lishe na ustawi wa vijana.

Mheshimiwa Zungu alieleza hayo Oktoba 8, 2026, wakati akitoa hotuba ya ufunguzi katika mdahalo kuhusu masuala ya afya ya mama na mtoto uliondaliwa na Serikali ya Tanzania kwa wajumbe wa Mkutano wa 153 Umoja wa Mabunge Duniani.

Mheshimiwa Spika alisema afya na ustawi wa wanawake, watoto na vijana ni msingi wa maendeleo ya Taifa na kwamba Tanzania inatarajia kuchangia uzoefu wake na kufanya kazi na washirika kugeuza dhamira ya kisiasa kuwa matokeo ya kudumu.

"Kila kifo kinachozuilika, kila hitaji la kiafya lisilotimizwa na kila kikwazo cha kupata huduma, kinahitaji umakini na hatua endelevu za kisiasa."

"Ndio maana Rais wangu Mhe. Rais Samia ameweka kipaumbele cha kupunguza vifo vya wajawazito, kupunguza vifo vya watoto na idadi ya watoto wasiochanjwa hadi sifuri, si tu nchini Tanzania bali pia kuchochea hatua hizi kote barani Afrika kupitia wadhifa wake kama Kinara wa Afya ya Mama na Mtoto Barani Afrika," amesema.

Alisema Bunge lina jukumu la kuendeleza sheria, kuhakikisha fedha za kutosha zinatengwa na kusimamia utekelezaji kuhakikisha rasilimali zinafika kwenye huduma za mstari wa mbele na kwa jamii.

"Kipaumbele chetu kiwe kwenye upatikanaji sawa wa huduma, ikiwemo huduma za mama

na mtoto mchanga, afya ya uzazi, lishe, na afya na ustawi wa vijana. Kupitia Mtandao huu, tunaweza kujifunza kutoka kwa kila mmoja, kuimarisha uwajibikaji wa kibunge na kuendeleza hatua za vitendo katika nchi zetu," alisema.

Kwa upande wake Mshauri wa Rais anayeshughulikia masuala ya afya, ustawi wa jamii, wanawake na watoto, Ummy Mwalimu aliyemwakilisha Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan, alisema Afrika imepiga hatua katika kupunguza vifo vya kina mama japo bado haijatosha.

Alisema vifo vya kina mama katika nchi wanachama wa Umoja wa Afrika vilipungua kwa asilimia 42 kati ya mwaka 2000 na 2023, lakini Afrika bado inachangia takribani asilimia 70 ya vifo vya kina mama duniani.

"Kwa kasi iliyopo sasa Afrika haitaweza kufikia lengo la Maendeleo Endelevu la kuwa na vifo vya kina mama 70 kwa kila vizazi hai 100,000 hadi karibu mwaka 2050," amesema Mwalimu. Mwenyekiti wa Kundi la Kijiografia la Afrika la IPU, Mhe. Ali Kolotou Tchaïmi alisema Wabunge wana wajibu wa kuhakikisha ahadi za afya zinawafikia wananchi wa kawaida.

Alisema watunga sheria wana jukumu la kutunga sheria, kuidhinisha bajeti na kusimamia serikali, hususan katika kulinda makundi yaliyo katika mazingira hatarishi.

Akitoa mchango wake katika mkutano huo, Spika wa Bunge la Afrika Kusini, Angela Thokozile Didiza, alitoa wito wa kuimarishwa kwa uongozi wa kisiasa, akibainisha kuwa vifo vya kina mama na chanjo za watoto bado ni changamoto kubwa za afya ya umma.

"Kila kifo kinachozuilika, kila hitaji la kiafya lisilotimizwa na kila kikwazo cha kupata huduma, kinahitaji umakini na hatua endelevu za kisiasa." Spika Zungu



AUSTRALIA ACHAGULIWA KUWA RAIS WA 32 WA UMOJA WA MABUNGE DUNIANI

Na Zuhura Mtatifikolo

Spika wa Baraza la Wawakilishi la Australia, Mhe. Milton Dick amechaguliwa kuwa Rais wa 32 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) katika Mkutano wa 153 wa IPU unaofanyika Arusha, Tanzania.

Uchaguzi huo ulifanyika katika Ukumbi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC) Oktoba 9, 2026.

Mhe. Dick alishinda kwa asilimia 56 ya kura zote, huku akifuatiwa na Prof. Mhe. Sahiba Gafarova aliyepata asilimia 38 na Mhe. Robi Edwards alipata asilimia sita.

Mhe. Dick anachukua nafasi ya Dkt. Tulia Ackson wa Tanzania, ambaye amemaliza muhula wake wa miaka mitatu.

Mhe. Dick ni Mbunge wa Jimbo la Oxley, Queensland tangu mwaka 2016, alichaguliwa kwa mara ya kwanza kuwa Spika mwaka 2022 na kuchaguliwa tena bila kupingwa mwaka 2025.

Baada ya kuchaguliwa Mhe. Dick amesisitiza umuhimu wa umoja na ushirikiano kwenye umoja huo.

"Leo hakuna mshindi wala mshindwa. IPU imeongea kwa sauti moja. Hii ndiyo demokrasia.

"Ni ukumbusho kuwa mazungumzo, heshima na ushirikiano bado vina umuhimu. Tutafanya kazi pamoja, tusikilizane, tutapata muafaka." amesema.

Mhe. Dick ataongoza mikutano ya kisheria ya IPU na kuiwakilisha taasisi hiyo katika matukio makubwa ya kimataifa, akifanya kazi kwa karibu na Katibu Mkuu Anda Filip.

Kuchaguliwa kwake kunaashiria sura mpya kwa IPU wakati wabunge wanaendelea kuimarisha majadiliano, uwakilishi wa kidemokrasia na ushirikiano wa kimataifa katika dunia inayokabiliwa na changamoto tata za kimataifa.



MHE. REMBO: UHIFADHI WA MAZINGIRA UWE CHANZO CHA FURSA ZA KIUCHUMI KWA VIJANA

Na. Said Mussa

Mbunge wa Viti Maalum ambaye pia ni Mjumbe wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) Mheshimiwa Fatma Rembo amehimiza mabunge kuimarisha sheria, bajeti na ushirikiano wa kimataifa kufanikisha lengo la kuhifadhi asilimia 30 ya maeneo ya asili ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Rembo alitoa wito huo wakati akichangia mjadala kuhusu mabadiliko ya tabianchi na uongozi wa kibunge katika kulinda mifumo ya ikolojia ya milima na bahari, wakati wa Mkutano wa 153 IPU uliofanyika jijini Arusha, Oktoba 5-9, 2026.

Mheshimiwa Rembo alisema mabunge duniani yanatakiwa kuhakikisha kuwa juhudi za kulinda mazingira, hususan mifumo ikolojia ya milima na bahari, zinaenda sambamba na fursa za ajira, uwezeshaji wa vijana na maendeleo endelevu ya kiuchumi.

Aidha alisisitiza umuhimu wa kubadili ahadi za uhifadhi wa mazingira kuwa hatua madhubuti zinazotekelezwa kupitia sheria, sera na bajeti. Alisema lengo la kuhifadhi asilimia 30 ya maeneo ya asili ifikapo mwaka 2030 linahitaji ushiriki wa jamii, uwekezaji wa kutosha na ushirikiano wa kimataifa, akibainisha kuwa uhifadhi haupaswi kuonekana kama kikwazo cha maendeleo, bali kama fursa ya kukuza uchumi na kuboresha maisha ya wananchi.

"Uhifadhi haupaswi kuonekana kama kikwazo cha maendeleo. Badala yake, ni uwekezaji katika maendeleo endelevu."

Mheshimiwa Rembo alieleza kuwa, milima na bahari ni rasilimali muhimu zinazotegemewa na mamilioni ya watu kwa ajili ya maji, chakula, ajira, kilimo, utalii, usafirishaji na shughuli nyingine za kiuchumi. Hata hivyo, rasilimali hizo zinazidi kukabiliwa na changamoto za mabadiliko ya tabianchi, uchafuzi wa mazingira, upotevu wa bioanuwai na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za asili.

Akizungumzia mazingira ya Tanzania, alisema nchi imebarikiwa kuwa na mifumo ikolojia muhimu, ikiwemo Mlima Kilimanjaro, Mlima Meru, misitu, makazi ya wanyamapori pamoja na ukanda wa pwani na visiwa vinavyounganishwa na mazingira mapana ya Bahari ya Hindi.

Alisisitiza kuwa ulinzi wa rasilimali hizo unahitaji kuhusisha wananchi wanaozitegemea katika maisha yao ya kila siku, ili wawe washiriki na wanufaika wa moja kwa moja wa shughuli za uhifadhi.

"Jamii zinapopata manufaa kutokana na uhifadhi, zinakuwa washirika imara zaidi katika kulinda rasilimali za asili." Alisema Mhe. Rembo

Katika kuimarisha nafasi ya vijana, Mheshimiwa Rembo alihimiza kuwepo kwa mifumo inayowawezesha vijana na wanawake kushiriki katika shughuli za kiuchumi zinazohusiana



na uhifadhi, ikiwemo utalii endelevu, kilimo kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi, nishati jadidifu, ubunifu wa teknolojia na uchumi wa buluu.

Alisema hatua hiyo ni muhimu kwa nchi zinazoendelea, ambako vijana wanahitaji ajira na fursa za kujipatia kipato huku nchi hizo zikiendelea kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Wajibu wetu kama wabunge si kupitisha maazimio pekee. Wajibu wetu ni kuhakikisha kwamba maazimio hayo yanatafsiriwa kuwa sheria, sera, bajeti na hatua zinazotekelezwa na ambazo matokeo yake yanaweza kupimwa." Mheshimiwa Rembo pia alisisitiza umuhimu wa matumizi ya sayansi na teknolojia za kisasa, ikiwemo uangalizi wa mazingira kupitia

satelaiti, utafiti wa kisayansi na teknolojia za kidijitali, katika kufuatilia mabadiliko ya misitu, milima, bahari na bioanuwai. Amesema juhudi hizo zinapaswa kuzingatia pia maarifa ya jamii za wenyeji na jamii za asili ambazo zimekuwa zikilinda rasilimali hizo kwa vizazi vingi.

Kupitia IPU, alisema, mabunge yana fursa ya kubadilishana uzoefu, sheria, mbinu bora na suluhisho bunifu, huku yakizitaka serikali kuwajibika katika kutekeleza ahadi zilizotolewa.

MKUTANO WA IPU KULETA NEEMA KWA WAKULIMA WA KAROTI ARUSHA

Na Patson Sobha

Faida zinazotokana na ujio wa wageni zaidi ya 2000 kutoka mataifa mbalimbali waliohudhuria Mkutano wa IPU wa 153, kwa wengi yanaangaliwa na kuonekana moja kwa moja kwenye mapato ya utalii, hoteli, chakula, usafiri, na mahusiano ya kibiashara na kidiplomasia. Hata hivyo, kwa wakulima wa karoti wa Wilaya ya Arumeru, wamepata neema ambayo hawakuitarajia.

Wakulima wa Klasta ya Karoti ya Kijiji cha Sura wanaoratibiwa na kusimamiwa na Taasisi Kilele ya Kilimo cha Mbogamboga na Matunda (TAHA) walipata neema ya kupokea ugeni huo baada ya kushauriwa na Mkurugenzi wa Taasisi hiyo. Wakulima hao walimpokea Rais wa Seneti akiambatana na Maseneta watatu, Wabunge wa Bunge la Wawakilishi la Thailand

watatu pamoja na watumishi wa Seneti na Bunge wanne, walipotembelea mashamba ya wakulima tarehe 9 Oktoba 2026.



Mgeni njoo, mwenyeji apone, ni msemo wa wahenga uliodhihirika kwa wakulima wa karoti wa Kijiji cha Sura, Kata ya Songoro, Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, pale walipotembelewa na Rais wa Seneti ya Thailand, Mhe. Mongkol Surasajja. Mgeni huyo na ujumbe wake waliokuwa wanahudhuria Mkutano wa IPU wa 153 uliofanyika kuanzia tarehe 5 – 9 Oktoba, 2026 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC), waliomba kupata fursa ya kuonana na wakulima wa Tanzania.

Mhe. Mongkol akiwa katika mashamba ya klasta ya karoti, alivutiwa sana na mashamba ya wakulima hao na kusifu jitihada za TAHA za kuwezesha uratibu wa mafunzo ya kitalaam na pia kuwaunganisha na masoko. Aidha, baada ya kujionea hali halisi ya kilimo hicho, aliahidi kuunda ushirikiano utakaowezesha kupata masoko ya karoti za Tanzania huko Thailand na kuwa na mpango wa kubadilishana uzoefu wa watalaam wa kilimo.

"Nimevutiwa sana na mashamba haya ya karoti nzuri na kubwa na za kupendeza ambazo kwa Thailand tunalima kiasi kidogo sana. Naamini tunaweza kuunda ushirikiano wa namna ya kupata masoko huko kwetu japo ni mbali, lakini pia tunaweza kuleta watalaam wa kilimo ili washirikiane na watalam wa Tanzania." Alisema Mhe. Mongkol.

Katika hatua nyingine, Balozi wa Thailand kwa nchi za Tanzania na Kenya mwenye ofisi yake jijini Nairobi, aliyeongozana na ujumbe huo, Mhe. Balozi Morakot Janemathukorn, alimwambia Mkurugenzi wa TAHA aandae andiko la kuunda ushirikiano wa kitalaam pamoja na namna wanavyohitaji Serikali ya Thailand iweze kusaidia kilimo cha karoti kwa wakulima wa Arumeru.

'Ningependa tuwasiliane na Mkurugenzi wa TAHA, ili aandae andiko la namna wanavyotaka tushirikiane kwa masuala ya utalaam wa kilimo pamoja na masoko ili kuwasaidia wakulima hawa. Baada ya kupokea andiko, nitawasiliana na Serikali ya Thailand ili kuona ni namna gani itaweza kusaidia". Alisema Balozi Morakot.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Sura, Sadiekiel Solomon, akiongea kwa niaba wa wakulima, alimshukuru Rais huyo wa Seneti pamoja na ujumbe wake kwa kuona umuhimu wa kuwatembelea. Alisema wamejisikia heshima na fahari kubwa sana kutembelewa na watu wakubwa na wametiwa moyo kwa ahadi zilizotolewa za kupata watalaam na kutafutiwa masoko, maana ndiyo changamoto kubwa inayowakabili.


Mkurugenzi wa TAHA, Dkt. Jacqueline Mkindi, alimshukuru Rais huyo wa Seneti ya Thailand, Balozi na ujumbe wao kwa kutembelea ofisi ya TAHA na mashamba pamoja na kutoa ahadi ambazo zimeongeza aari na matumaini kwa wakulima wa eneo hilo. Aliahidi kuandaa andiko mapema iwezekanavyo na kulituma kwa Balozi kama walivyoelekezwa ili wakulima wa karoti wa Arumeru waweze kunufaika na kilimo hicho.

Awali, Rais wa Seneti ya Thailand, alitembelea Kituo cha Mafunzo ya Kilimo cha Tengeru kinachosimamiwa na TAHA, ambapo alijionea mashamba ya ndizi zinazolimwa kwa umwagiliaji wa kisasa. Aidha, alitembelea jengo la ofisi ya shamba hilo lenye vyumba maalum vya kuhifadi matunda na sehemu ya kufungashia kitalaam kabla ya kusafirisha kwenda kwenye masoko ya ndani na nje ya Tanzania.

Mhe. Mongkol amepata umaarufu kule Thailand kwa kuwa mkulima hodari anayemiliki mashamba katika Jimbo la Buri Ram. Sifa hiyo ndiyo imempa nafasi ya kuchaguliwa kuwa Seneta kutoka kundi la wakulima mwezi Juni 2024 kati ya wagombea 20 wa makundi mbalimbali, na baadaye akachaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa Seneti Julai 2024.

Baada ya utumishi wake wa muda mrefu katika Serikali ya Thailand, ambako alitumikia kama Gavana wa Jimbo la Buri Ram na Mkurugenzi wa Mkuu wa Utawala wa Jimbo, aliwekeza kwenye kilimo cha mbogamboga na ufugaji wa samaki, shughuli ambayo anaahidi kuendelea kuitekeleza hata atakakuwa amemaliza muda wake wa nafasi ya Rais wa Seneti.

Kwa Mhe. Mongkol, kilimo ndiyo maisha maana anasema kiko ndani ya damu yake, na ameanza kulima tangu enzi za utoto akiwa na babu yake pamoja na baba yake. Aidha, amekuwa kinara wa kuhamasisha kilimo kupitia mipango ya Seneti ya kuwafikia wakulima ukiwemo Mpango wa "Wathailand Kusaidia Wathailand (Thais Help Thais)," mpango unaotoa misaada kwa wakulima wadogo wenye hali duni.





Dkt. Zeyana Achaguliwa Kuiwakilisha Tanzania Kamati ya Afya ya IPU

Na Theresia Rugemalila

Mbunge wa Viti Maalum kutoka Zanzibar, Mhe. Dkt. Zeyana Abdallah Hamid, amechaguliwa kuiwakilisha Tanzania katika Kamati ya Afya ya Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) kwa kipindi cha miaka minne, kuanzia mwaka 2026 hadi 2029, baada ya kupata kura 63 katika uchaguzi uliofanyika wakati wa Mkutano wa 153 wa IPU jijini Arusha.

Katika uchaguzi huo uliofanyika Oktoba 9, 2026, wakati wa mkutano wa 153 wa IPU uliofanyika kuanzia Oktoba 5 hadi 9, 2026, Dkt. Zeyana alishindana na wagombea kutoka nchi za Pakistan, Monaco na Niger.

Uchaguzi huo unampa Dkt. Zeyana fursa ya kushiriki katika mijadala ya kimataifa kuhusu sera na mifumo ya afya, huku ukiiongezea Tanzania nafasi ya kuwasilisha vipaumbele vyake katika jukwaa la kibunge la kimataifa na kujifunza kutokana na uzoefu wa nchi nyingine katika kukabiliana na changamoto za sekta hiyo.

Kamati ya Afya ya IPU ni jukwaa linalowawezesha wabunge kujadili masuala ya afya kwa kuzingatia sheria, sera za umma, usimamizi wa rasilimali na ushirikiano wa kimataifa. Kupitia uwakilishi huo, Tanzania itapata fursa ya kushiriki katika mazungumzo kuhusu namna mabunge yanavyoweza kuchangia kuimarisha huduma za afya na mifumo ya utoaji huduma kwa wananchi.

Kwa Tanzania, sekta ya afya ni eneo muhimu linalohitaji uwekezaji endelevu katika miundombinu, dawa na vifaa tiba, wataalamu wa afya pamoja na usimamizi bora wa rasilimali. Hivyo, ushiriki katika majukwaa ya kimataifa unaweza kupanua wigo wa mijadala kuhusu changamoto hizo na mbinu zinazoweza kutumika kukabiliana nazo.

Moja ya manufaa yanayoweza kupatikana ni kujifunza kutokana na uzoefu wa nchi nyingine katika kutunga na kusimamia sera za afya. Mijadala ya kimataifa inaweza kusaidia kubaini mbinu bora zinazoweza kuzingatiwa katika mazingira ya Tanzania, kwa kuzingatia uwezo wa kiuchumi, mahitaji ya wananchi na vipaumbele vya maendeleo ya taifa.

Nchi nyingi zinakabiliwa na changamoto za kuhakikisha huduma bora za afya zinapatikana kwa wananchi wa mijini na vijijini, kupunguza gharama za matibabu na kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Ushiriki katika majadiliano kuhusu changamoto hizo unaweza kuisaidia Tanzania kupata mitazamo

mipya kuhusu namna ya kuboresha mipango na utoaji wa huduma za afya.

Aidha, uzoefu utakaopatikana katika majukwaa hayo unaweza kuwa na manufaa katika mijadala ya Bunge kuhusu bajeti za afya, usimamizi wa matumizi ya fedha za umma na ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera. Wabunge wana wajibu muhimu wa kuhakikisha rasilimali zinazotengwa kwa ajili ya afya zinatumika kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kwa msingi huo, uwakilishi wa Dkt. Zeyana unaweza kuwa daraja kati ya mijadala ya kimataifa na majadiliano ya kisera nchini. Hata hivyo, manufaa hayo yatategemea mawasiliano na taasisi husika, pamoja na kuwasilisha uzoefu na mapendekezo yanayopatikana katika majukwaa hayo kwa ajili ya kujadiliwa na kuzingatiwa katika mazingira ya Tanzania.

Mbali na kuchaguliwa katika Kamati ya Afya, Dkt. Zeyana alipewa pia jukumu la kuwa Rais wa Mkutano wa Awamu ya 42 wa Jukwaa la Wabunge Wanawake (Forum of Women Parliamentarians). Nafasi hiyo inampa jukumu jingine la uongozi katika mijadala ya kimataifa kuhusu ushiriki wa wanawake katika siasa na shughuli za kibunge.

Uongozi wake katika jukwaa hilo unatoa fursa ya kuendeleza mijadala kuhusu afya ya wanawake na wasichana, afya ya uzazi, lishe, usawa katika upatikanaji wa huduma na nafasi ya wanawake katika kufanya maamuzi ya kisera.

Masuala hayo yana umuhimu mkubwa katika maendeleo ya jamii, kwani upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wanawake na wasichana una mchango katika ustawi wa familia na jamii kwa ujumla. Vilevile, kuimarisha ushiriki wa wanawake katika uongozi na maamuzi kunaweza kusaidia kuhakikisha mahitaji yao yanazingatiwa katika uandaaji na utekelezaji wa sera.

Kwa Tanzania, nafasi hizo mbili zinaweza kuchangia kuimarisha diplomasia ya kibunge na mahusiano na wabunge kutoka mataifa mengine. Ushirikiano huo unaweza kuwezesha kubadilishana uzoefu, kujenga mawasiliano na kuendeleza mazungumzo kuhusu changamoto zinazokabili mifumo ya afya duniani.

Hata hivyo, masuala ya afya yanahitaji mipango na ushirikiano wa taasisi mbalimbali, zikiwemo Serikali, wataalamu wa afya na wadau wa maendeleo. Nafasi ya Dkt. Zeyana inaweza kuwa na tija zaidi iwapo changamoto



zinazowakabili wananchi zitawasilishwa katika mijadala husika na mapendekezo yanayofaa kwa mazingira ya Tanzania yakafuatiliwa na kujadiliwa na taasisi za ndani.

Kwa ujumla, manufaa ya muda mrefu yatategemea uwezo wa kuunganisha mijadala ya kimataifa na mahitaji ya wananchi wa maeneo mbalimbali, hususan jamii zilizo katika mazingira magumu au zenye upatikanaji mdogo wa huduma za afya.

Ni muhimu kutambua kuwa ushirikiano wa kimataifa hauleti matokeo wenyewe. Ili nafasi hizo ziwe na manufaa, zinahitaji malengo yanayopimika, mawasiliano ya mara kwa mara na wadau wa ndani, pamoja na ufuatiliaji wa mapendekezo yanayoweza kutekelezwa.

Katika kipindi cha miaka minne cha uwakilishi wake, matarajio ni kuona uzoefu na mijadala ya kimataifa ikiunganishwa na vipaumbele vya ndani ili kuchangia juhudi za kuboresha huduma za afya na kuimarisha ushiriki wa wanawake katika uongozi.

Afya bora ina uhusiano mkubwa na maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Wananchi wanapopata huduma za afya kwa wakati, wana nafasi kubwa zaidi ya kushiriki katika shughuli za uzalishaji, elimu na maendeleo ya jamii. Kwa upande mwingine, magonjwa yanayozuilika, gharama kubwa za matibabu na upungufu wa huduma vinaweza kuongeza mzigo kwa familia na kuathiri uwezo wao wa kujikwamua kiuchumi.

Kwa hiyo, mijadala inayolenga kuimarisha mifumo ya afya inaweza kuchangia maendeleo ya muda mrefu iwapo itasaidia kuibua sera na hatua zinazotekelezeka. Tanzania inaweza kutumia fursa hiyo kujifunza kuhusu usimamizi wa rasilimali, upangaji wa huduma kulingana na mahitaji ya wananchi na umuhimu wa kuweka mifumo imara ya uwajibikaji.



BUNGE: SAMIA AMEIPA TANZANIA HESHIMA DUNIANI

Na Zuhura Mtatifikolo

BUNGE limempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuiwezesha Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU).

Limesema hatua hiyo imeiandikia nchi historia, kuimarisha heshima yake kimataifa na kufungua fursa mpya za ushirikiano wa kidiplomasia na mataifa mbalimbali.

Pongezi hizo ziliwasilishwa bungeni na Mbunge wa Mtama, Mhe. Nape Nnauye, kupitia Azimio la Bunge la kumpongeza Mhe. Rais Samia kwa kuridhia na kuwezesha mkutano huo uliofanyika jijini Arusha kuanzia Oktoba 5 hadi 9, mwaka huu.

Mhe. Nape alisema Tanzania imeandika historia kwa kuwa mwenyeji wa mkutano huo kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa IPU mwaka 1889.

Alibainisha kuwa mafanikio ya maandalizi na uendeshaji wake yameonesha uwezo wa nchi kuandaa mikutano mikubwa ya kimataifa na kuwa jukwaa la majadiliano kuhusu masuala yanayoigusa dunia.

Alisema kuwa mafanikio hayo ni kielelezo cha kazi iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Rais Samia katika kuimarisha misingi ya utawala bora na diplomasia ya Tanzania duniani.

Kwa mujibu wa Mhe Nape, kuaminiwa kwa Tanzania na taasisi hiyo muhimu ya kimataifa kuandaa mkutano huo ni heshima kubwa kwa taifa na uthibitisho wa nafasi yake katika kukuza amani, demokrasia, utawala bora na ushirikiano baina ya mataifa.

Alisema pamoja na kuwa katika kipindi cha maombelezo ya msiba wa mumewe, Rais Samia alionesha ustahimilivu na uzalendo kwa kutoa ushirikiano kamili uliowezesha mkutano huo wa kihistoria kufanyika kwa mafanikio makubwa.

"Naomba kutoa pongezi za dhati kwa Rais wetu mpendwa kwa uongozi wake uliotukuka na wa makini uliowezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa. Pamoja na kuwa kwenye maombolezo ya msiba wa mume wake mpendwa, tunamwomba Mwenyezi Mungu ampe pumziko la amani, bado alionesha ustahimilivu na uzalendo mkubwa katika kipindi hiki kigumu," ameeleza Mhe. Nape.

Mhe. Nape alisema mkutano huo haukuwa

tukio la kawaida la kimataifa, bali ulikuwa fursa ya Tanzania kuonesha uwezo wake wa kuratibu mikutano mikubwa na kuthibitisha dhamira yake ya kushirikiana na mataifa mengine katika kutafuta majibu ya changamoto zinazoukabili ulimwengu.

Akieleza mafanikio ya mkutano huo, Mhe. Nape alisema ulihudhuriwa na washiriki 2,044 kutoka zaidi ya nchi 150, wakiwemo Maspika 56, Manaibu Spika 51 na Wabunge 624, pamoja na watumishi wa mabunge, Sekretarieti ya IPU na wanahabari.

Alisema ushiriki huo wa viongozi wa mabunge kutoka sehemu mbalimbali duniani umefungua fursa za kuimarisha mahusiano kati ya Bunge la Tanzania na mabunge ya mataifa mengine, huku ukiipa nchi nafasi ya kuonesha uwezo wake katika diplomasia ya kibunge.

Miongoni mwa viongozi waliohudhuria mkutano huo ni Spika wa Bunge la Uingereza, Sir Lindsay Hoyle, ambaye kwa mujibu wa Mhe. Nape alitembelea Tanzania kwa mara ya kwanza na kupata nafasi ya kujionea hali ya amani, utulivu na maendeleo yanayofanyika nchini.

Alisema kiongozi huyo alionesha kufurahishwa na hali hiyo na kuahidi kurejea tena Tanzania, jambo linaloonesha umuhimu wa wageni kupata fursa ya kujionea wenyewe hali halisi ya nchi badala ya kutegemea taarifa wanazozipata kutoka vyanzo vingine.

Nape amesema mojawapo ya mafanikio makubwa ya mkutano huo ni kusaidia kubadilisha mtazamo kuhusu Tanzania, kwa kuwa wajumbe wa kimataifa walipata nafasi ya kujionea amani, usalama na maendeleo yaliyopo nchini.

Alieleza kuwa wageni hao watakuwa mabalozi wazuri wa kuieleza dunia kuhusu hali halisi ya Tanzania na hivyo kuchangia kuimarika kwa uelewa na mahusiano kati ya nchi hiyo na mataifa wanakotoka.

ARUSHA YANUFAIKA KIUCHUMI

Mbunge huyo alisema mkutano huo umechangia uchumi wa taifa, hususan jijini Arusha, kupitia sekta za hoteli, usafiri wa anga, biashara na ajira.

Alieleza kuwa uwepo wa wajumbe na wageni wengi ulizipa hoteli za Arusha fursa ya kuhudumia washiriki, hali iliyoongeza shughuli za kiuchumi katika sekta hiyo.

Aidha, alisema mahitaji ya safari za ndege kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) na Uwanja wa Ndege wa Arusha yalitoa fursa kwa watoa huduma za usafiri kupata mapato kutokana na safari za wageni na shughuli zilizohusiana na mkutano huo.

Aliongeza kuwa wafanyabiashara wadogo na wa kati, wakiwemo wauzaji wa chakula na wajasiriamali wanaouza bidhaa za utalii, walipata fursa ya kuwafikia wateja wa kimataifa na kunufaika na shughuli za mkutano huo.



Mhe. Nape alisema mafanikio hayo yanaonesha kuwa kuandaa mikutano mikubwa ya kimataifa kunaweza kutoa fursa za kukuza shughuli za kiuchumi, kutangaza vivutio vya nchi na kupanua wigo wa biashara kwa wajasiriamali wa ndani.

ARUSHA KUIMARIKA KAMA KITOVU CHA DIPLOMASIA

Akizungumzia nafasi ya Arusha, Mhe. Nape alisema jiji hilo si kitovu cha mikutano pekee, bali pia lina historia muhimu katika harakati za ukombozi wa Afrika, ushirikiano wa kikanda, haki za binadamu na juhudi za kutafuta suluhu za migogoro kwa njia ya mazungumzo.

Alisema Arusha ni makao makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na eneo ilipo Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, hivyo kufanyika kwa mkutano huo kumeongeza fursa za kulitangaza jiji hilo kama

kitovu cha diplomasia, majadiliano ya kimataifa na ushirikiano wa mabunge.

Kupitia azimio hilo, Bunge lilihimiza juhudi endelevu za Rais Samia katika kuitangaza na kuiendeleza Arusha kama kitovu cha mikutano mikubwa, utalii, diplomasia na ushirikiano wa kimataifa.

Hatua hiyo inalenga kuendeleza nafasi ya Tanzania katika kupokea mikutano ya kimataifa na kutumia fursa zinazotokana na wageni wanaotembelea nchi kwa shughuli za kidiplomasia, biashara na utalii.



AMANI, DEMOKRASIA NA HAKI ZA BINADAMU

Mhe. Nape alisema mkutano wa IPU ulitoa jukwaa la majadiliano kuhusu amani, usalama, demokrasia, haki za binadamu na utatuzi wa migogoro kwa njia za amani, katika kipindi ambacho dunia inakabiliwa na changamoto mbalimbali.

Alitaja changamoto hizo kuwa ni pamoja na migogoro ya kivita, migawanyiko ya kisiasa, mabadiliko ya tabianchi na kupungua kwa imani ya wananchi kwa baadhi ya taasisi za umma.

Alisema majadiliano yaliyofanyika yamesisitiza umuhimu wa diplomasia ya kibunge, kuheshimu sheria za kimataifa na kuimarisha taasisi za kidemokrasia ili ziweze kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi.

Aliongeza kuwa mijadala kuhusu haki za binadamu, watu wenye ulemavu, mabadiliko ya tabianchi na teknolojia zinazoibukia imeonesha wajibu wa mabunge katika kutafuta majibu ya changamoto zinazowakabili wananchi.

Kwa mujibu wa Nape, ushirikiano wa mabunge ni muhimu katika kujenga misingi ya maelewano baina ya mataifa na kutafuta suluhu zinazozingatia maslahi ya wananchi na maendeleo ya binadamu.

USHIRIKI WA WANAWAKE WAFIKIA ASILIMIA 39.4

Katika eneo la ushiriki wa wanawake, Mhe. Nape alisema mkutano huo uliweka rekodi ya ushiriki wa wanawake waliofikia asilimia 39.4 ya wabunge waliohudhuria.

Alisema kiwango hicho kinaonesha umuhimu wa kuendelea kupanua nafasi za wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika uongozi na maamuzi, ili kuhakikisha makundi hayo yanashiriki kikamilifu katika masuala yanayohusu maendeleo ya jamii.

Amesema kitendo cha Umoja wa Mabunge Duniani ya kuamua kuipa heshima Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa 153 wa IPU ni matokeo ya kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kuimarisha misingi ya utawala bora na diplomasia ya Tanzania Duniani.

Alieleza kuwa ushiriki jumuishi ni sehemu muhimu ya kuimarisha demokrasia na utawala bora, kwa kuwa unatoa nafasi kwa makundi mbalimbali kuchangia katika maamuzi na mijadala inayohusu mustakabali wa wananchi.

TAMKO LA ARUSHA LATOA MWELEKEO

Mhe. Nape alisema mkutano huo umeacha urithi muhimu kupitia Tamko la Arusha, linalosisitiza utawala bora, ushirikishwaji, uaminifu na fursa kwa wote.

Alisema thamani ya demokrasia haipimwi kwa uwepo wa taasisi pekee, bali pia kwa namna taasisi hizo zinavyoboresha maisha ya wananchi kupitia maamuzi na utekelezaji wa sera zinazowagusa.

Alieleza kuwa mafanikio ya mkutano huo hayapaswi kuishia katika kutoa pongezi pekee, bali yanapaswa kuendelezwa kupitia sheria bora, uwajibikaji, usimamizi wa Serikali na ushirikishwaji wa wananchi.



Mkutano huo pia ulijadili masuala mbalimbali yaliyojumuishwa katika maazimio yake, yakiwemo kuimarisha utawala bora na kuwezesha jamii kupitia ujumuishi, uaminifu na fursa kwa wote; maendeleo ya kijamii jumuishi; mikakati ya kibunge ya kukuza haki na uwezeshaji wa watu wenye ulemavu; na hatua za haraka za kukabiliana na majanga yanayohusiana na tabianchi.

Masuala mengine ni kukuza mustakabali wa kazi unaozingatia haki, ujumuishi na uendelevu katika kipindi cha maendeleo ya akili unde (AI), pamoja na kujadili namna Umoja wa Mataifa unavyoweza kukidhi mahitaji ya wakati huu.

Kwa mujibu wa azimio hilo, masuala hayo yanaendana na vipaumbele vya uongozi wa Mhe. Rais Samia katika kuimarisha ushirikiano wa kimataifa, demokrasia na maendeleo jumuishi.

Mhe. Nape alitoa pongezi pia kwa Spika wa Bunge Mussa Zungu, Katibu wa Bunge, Baraka Leonard, na Kamati nzima ya Maandalizi kwa kazi ya kuongoza na kuratibu maandalizi yaliyowezesha mkutano huo kufanyika kwa mafanikio.

Alisisitiza kuwa mafanikio ya Tanzania katika mkutano huo yanapaswa kuwa mwanzo wa kuendeleza ushirikiano uliojengwa, mawazo yaliyotolewa na maamuzi yaliyofikiwa ili kuchangia maendeleo ya taifa na dunia kwa ujumla.

KAULIYA MHE. SPIKA

Spika wa Bunge, Mhe. Mussa Zungu, amesema kufanyika kwa Mkutano Mkuu wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) kwa hapa nchini ni ishara ya imani ya jumuiya ya kimataifa kwa Tanzania, akiwataka Watanzania kulinda amani na kuepuka migogoro isiyo na tija ili kuendeleza heshima hiyo lakini wajiepushe maneno ya kejeli na kubeza.

Mhe. Zungu alisema mafanikio ya mkutano huo yameipa Tanzania nafasi ya kuonyesha maendeleo yake na uwezo wa kuandaa mikutano mikubwa ya kimataifa, huku viongozi waliohudhuria wakipata fursa ya kutambua hatua zinazopigwa katika sekta za afya, maji, umeme na miundombinu ambavyo anasema wengi walifurahia.

Spika alisema juhudi za Mhe. Rais Dkt. Samia katika kuitangaza Tanzania na kuimarisha mahusiano ya kimataifa zimechangia kufungua fursa za utalii na uwekezaji, akitaja filamu ya The Royal Tour kuwa sehemu ya mikakati ya kuitangaza nchi duniani.



Hata hivyo Spika alimpongeza Rais kwa kuendelea kuwa na uvumilivu lakini akabainisha kuwa, Tanzania haiwezi kujengwa kwa chama kimoja, badala yake milango iko wazi kwa vyama vingine kuungana kwenye ujenzi wa Taifa moja lenye amani na utulivu.

Alibainisha kuwa Serikali inaendelea kuimarisha ushirikiano na mashirika ya ndege ili kuongeza watalii wanaofika nchini, hatua inayotarajiwa kuchochea shughuli za kiuchumi na kuongeza fursa za ajira kwa wananchi, hasa vijana.

Akizungumzia uwekezaji, Mhe. Zungu alisema Tanzania inapaswa kuvutia miradi yenye manufaa kwa pande zote, huku masilahi ya taifa yakilindwa. Miongoni mwa miradi aliyosema imeliletea heshima Taifa ni pamoja na mradi wa gesi wenye thamani ya dola za Marekani bilioni 42 kuwa sehemu ya fursa kubwa zinazoweza kuchangia ukuaji wa uchumi na kuongeza ajira. Alisisitiza kuwa maendeleo ya taifa yanahitaji ushirikiano wa Watanzania wote bila kujali tofauti zao, akisema migogoro isiyo na tija inaweza kuathiri juhudi za kujenga uchumi na kuimarisha nafasi ya Tanzania kimataifa.

"Tanzania haiwezi kujengwa na chama kimoja,lazima tushirikiane kujenga Tanzania yetu kwa pamoja," alisema Mhe. Zungu, huku akiwashukuru wananchi wa Arusha, vyombo vya habari na vyombo vya ulinzi na usalama kwa mchango wao katika kufanikisha mkutano huo.

WABUNGE WAUNGA MKONO

Mbunge wa Nzega Mjini Mhe. Hussein Bashe yeye alisema mambo yaliyofanyika katika kipindi cha Rais Samia, ni mafanikio makubwa na yanaijenga Tanzania katika anga ya Kimataifa na kwamba amekuwa kiongozi wa kampeni za Watanzania wanaogombea nafasi mbalimbali za Kimatifa.

"Miaka michache iliyopita wakati Dkt Tulia Ackson (Spika Mstaafu), alipogombea nafasi ya Rais wa IPU, Marehemu Dkt Faustine Ndugulile na Profesa Janabi maeneo yote Rais alikuwa anapiga simu kwa viongozi wenzake kufanya kampeni, kwa hili lazima tupongeze," amesema Bashe.

Kwa upande wake Mbunge wa Arusha Mjini Paul Makonda amesema Mkutano huo umeibeba na kuutangaza mji wao akiomba mikutano ya Kimataifa kama huo iendelee kupelekwa katika Jiji hilo kwani inatoa matokeo yenye tija.

Makonda amesema katika kipindi hiki Serikali imeamua kujenga ukumbi wa hadhi ya kubeba zaidi ya watu 5,000 kwa wakati mmoja ili kuipeleka Tanzania katika ndoto ya kuingiza fedha nyingi kupitia mikutano kama ilivyo kwa nchi ya Thailand.

Mbunge wa Bunda Mjini Mhe. Ester Bulaya yeye anasema baadhi ya watu walikuwa wanaibeza Tanzania kwa wakati ule lakini sasa wamezibwa midomo kutokana na Diplomasia iliyopo na jinsi Rais Samia anavyoliongoza Taifa hili.

Bulaya amesema ni wakati wa kutembea kifua mbele na kujivunia kama Mtanzania kutokana na yanayofanyika ndani ya taifa lakini akawasifu wabunge wa IPU kutoka Bunge la Tanzania kwa namna walivyokuwa wawakilishi wazuri.



Akichangia Azimio hilo, Mbunge wa Hanang, Mhe. Asia Halamga alisema mkutano huo umeongeza fursa za kiuchumi na kuitangaza Tanzania kimataifa, huku akitaja pia nafasi ya Dkt. Tulia Ackson kuwa Rais wa IPU kama sehemu ya mafanikio ya Watanzania hususani wanawake.



Halamga alisema amani na utulivu ni msingi wa mafanikio hayo, hivyo akawataka Watanzania, hususan vijana, kushiriki katika kulinda amani na kuepuka vitendo vinavyoweza kuvuruga mshikamano wa taifa uliojengwa kwa misingi imara.

"Serikali imeendelea kuwawezesha vijana kupitia fursa za elimu na kuwaunga mkono wanaoiwakilisha Tanzania kimataifa, kila Mtanzania ana wajibu wa kuilinda nchi na kushiriki katika kujenga taifa lenye maendeleo na uchumi imara,"amesema Halamga.

Mbunge wa Kisarawe Mhe. Dkt Seleman Jafo alisema tukio hilo limeipa nchi jukwaa la kujitangaza na kuzungumza na mataifa mbalimbali ambao wengi hawakuijua Tanzania kwa ndani.

Dkt. Jafo alisema Tanzania ina malengo ya kufikia pato la taifa la dola za Marekani bilioni 117 na ukuaji wa uchumi wa asilimia 7.2 ifikapo mwaka 2030, sambamba na kuongeza idadi ya watalii hadi milioni nane, hivyo mkutano wa IPU ni moja ya mikakati ya kufikia malengo hayo kutokana na mambo waliyoyaona watalii.

Alisisitiza kuwa Watanzania wanapaswa kutunza heshima iliyopatikana kupitia mkutano huo kwa kuendeleza amani na mshikamano wa kitaifa, akieleza kuwa mkutano huo ulikuwa fursa muhimu ya kuitangaza Tanzania na kuimarisha uhusiano wake na dunia.

Naye Mbunge wa Same Mashariki Mhe. Anne Malecela alisema wananchi na viongozi wa Arusha wanastahili pongezi kwa mchango wao katika kuhakikisha wageni wanapata huduma na mazingira mazuri wakati wa mkutano huo.

Kwa mujibu wa Mhe. Kilango, mafanikio hayo yamewapa Watanzania sababu ya kujivunia nchi yao na kuonesha uwezo wa Tanzania kuandaa mikutano mikubwa ya kimataifa lakini akawapongeza wananchi wa Arusha kwa namna walivyoonyesha utulivu wakati wote wa kipindi cha Mkutano huo.

Kwa upande wake Mbunge wa viti Maalum, Mhe. Zainab Abdallah Issa alisema mkutano huo uliowakutanisha washiriki zaidi ya 2,000 umefungua fursa za kiuchumi kupitia sekta za usafiri, hoteli na utalii, huku wageni wakipata nafasi ya kutembelea vivutio mbalimbali nchini ambavyo wanakwenda kuvitangaza kwao.

Alibainisha kuwa, Tanzania ina nafasi ya kuimarika kama kitovu cha utalii na mikutano ya kimataifa, akimhimiza Rais kuendelea na juhudi za kuimarisha diplomasia ya uchumi kwani matokeo mazuri yameonekana.

Katika mchango wake Mbunge wa Mlalo, Mhe. Rashid Shangazi alisema mkutano huo umeitangaza Tanzania kupitia ukarimu, utamaduni na vyakula vya asili vilivyowavutia wageni, sambamba na kuwapa fursa ya kuwapa fursa ya kutembelea vivutio vya utalii.

Mhe. Shangazi aliwataka watendaji walioshiriki kufanikisha mkutano huo kutambuliwa kwa mchango wao, akisisitiza kuwa mafanikio hayo yameimarisha taswira ya Tanzania na kufungua fursa za kiuchumi kwani baada ya mkutano huo, matokeo mazuri yataonekana.

Akihitimisha hoja hiyo, Mhe. Nape alisema Watanzania hawapaswi kuruhusu watu wachache kuharibu historia na heshima ya nchi, akisisitiza umuhimu wa kulinda amani, umoja na utulivu ulioifanya Tanzania kuaminiwa na jumuiya ya kimataifa.

Nape anasema kufanyika kwa Mkutano Mkuu wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) nchini ni uthibitisho wa imani hiyo, kwani wajumbe kutoka mataifa mbalimbali walifika na kushiriki mkutano huo hadi kukamilika salama wataendelea kuwa mabalozi wema.

Alibainisha kuwa amani na utulivu ni mtaji wa taifa unaopaswa kulindwa na kila Mtanzania lakini alisema uongozi, uzalendo na ujasiri wa Rais Dkt. Samia vimechangia kuipa Tanzania heshima duniani, akieleza kuwa ujio wa IPU nchini ni sehemu muhimu ya historia ya awamu ya sita.

Alisisitiza kuwa Watanzania wanapaswa kushikamana na kuwapuuza wanaobeza maendeleo ya nchi kwa hatua ambayo Serikali ya awamu ya sita imepiga licha ya baadhi ya watu wanaoendelea kubeza lakini haisaidii kurudisha nyuma jitihada hizo

HADITHI YA BABU: AZIMIO LA BUNGE, UONGOZI NA SAFARI YA KUGEUZA HESHIMA YA KIMATAIFA KUWA MANUFAA KWA TAIFA

Na. Athuman Hussein, *ndc*
a.brambati@bunge.go.tz

Jioni moja, baada ya chakula cha usiku, babu aliketi chini ya mti mkubwa uliokuwa mbele ya nyumba yake. Wajukuu wake walimzunguka kwa hamu, wakisubiri hadithi ya siku hiyo. Babu akatabasamu na kusema, "Leo sitakusimulieni hadithi ya mfalme wala ya vita, bali ndoto iliyonifundisha jambo muhimu kuhusu Rais wetu, Bunge letu na maslahi ya taifa."

"Katika ndoto hiyo," babu alianza, "nilijikuta ndani ya Ukumbi wa Bunge la Tanzania. Wabunge walikuwa wameketi wakisikiliza hoja muhimu iliyowasilishwa na Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge wa Mtama, kuhusu Azimio la Bunge la kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mchango wake katika kufanikisha Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani, unaojulikana kama IPU." "Babu, azimio ni nini?" mjukuu mmoja akauliza. Babu akamjibu, "Azimio ni njia rasmi ambayo Bunge hutumia kueleza msimamo wake kuhusu jambo fulani. Bunge linapopitisha azimio la pongezi, linatambua mchango au mafanikio ambayo linaona yana umuhimu kwa taifa."

Babu akanyamaza kidogo, kisha akaendelea, "Kilichonivutia katika ndoto yangu ni kwamba pongezi hizo hazikuhusu mtu mmoja pekee, bali pia nafasi ambayo Tanzania ilipata mbele ya jumuiya ya kimataifa. Kuwa mwenyeji wa mkutano mkubwa wa mabunge duniani kunahitaji maamuzi, maandalizi na uratibu wa taasisi mbalimbali." Alitazama wajukuu wake na kuongeza, "Hapo ndipo nilipoanza kujiuliza kama thamani ya tukio kama hilo inaishia katika kulifanikisha au inaendelea pia katika namna taifa linavyotumia fursa zinazotokana nalo."

"Kwa hiyo, babu, Rais aliona mbali?" mjukuu mwingine akauliza. Babu akajibu, "Uamuzi wa kuunga mkono juhudi za Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano wa kimataifa unaweza kutazamwa kama hatua yenye umuhimu wa kimkakati. Thamani yake huonekana zaidi pale nafasi hiyo inaposaidia kujenga uhusiano wa kimataifa, kufungua fursa za ushirikiano na kuimarisha nafasi ya nchi katika majadiliano ya dunia."

Babu akaendelea, "Hata hivyo, kuwa mwenyeji wa mkutano si mwisho wa safari, bali ni mwanzo wa jukumu la kuhakikisha kwamba fursa zinazojitokeza zinageuzwa kuwa manufaa ya kudumu kwa taifa." Alipokuwa akitafakari jambo hilo katika ndoto yake, alijikuta akiwa Arusha, ambako mkutano ulikuwa ukiendelea.

"Niliona wageni kutoka nchi mbalimbali, magari yakisafirisha wajumbe, hoteli zikipokea wageni na wafanyabiashara wakihudumia wateja wao," babu akaendelea kusimulia. "Nilipozitazama shughuli hizo, nilijiuliza kama uwepo wa wageni hao ungeweza kuleta manufaa kwa wananchi wa Arusha, hasa wale ambao hawakuhusika moja kwa moja katika mkutano."

"Babu, ni kwa namna gani wananchi wangeweza kunufaika?" mjukuu mmoja akauliza. Babu akamjibu, "Mkutano wa aina hiyo unaweza kuongeza mahitaji ya malazi, chakula, usafiri na huduma nyingine, hivyo kufungua fursa kwa wafanyabiashara na watoa huduma. Hata hivyo, ili kujua manufaa halisi yaliyopatikana, ni muhimu kuchunguza matokeo yake, yakiwemo mapato, ajira na ushiriki wa biashara za ndani."

Babu akanyamaza kidogo, kisha akaendelea, "Lakini mwanangu, nilitambua kwamba thamani ya mkutano huu haikuishia katika shughuli za kiuchumi za Arusha. Kwa Tanzania, ulikuwa pia fursa ya kuimarisha nafasi yake katika ushirikiano wa kimataifa kwa kuwakutanisha viongozi wa mabunge kutoka sehemu mbalimbali za dunia." Hapo ndipo babu alipoanza kutafakari umuhimu mpana wa kuwa mwenyeji wa mkutano wa Umoja wa Mabunge Duniani, unaojulikana kama IPU.

"Babu, IPU ni taasisi ya aina gani, na kwa nini kuwa mwenyeji wa mkutano wake kulikuwa muhimu kwa Tanzania?" mjukuu mwingine akauliza. Babu akamjibu, "IPU ilianzishwa mwaka 1889 kwa lengo la kuimarisha mazungumzo na ushirikiano kati ya mabunge. Kuwa mwenyeji wa Mkutano wake wa 153 kuliipa Tanzania nafasi ya kuonesha uwezo wake wa kuandaa mikutano ya kimataifa, kuimarisha uhusiano na mabunge mengine na kutambua fursa za ushirikiano wa baadaye." Alisisitiza kwamba thamani ya nafasi hiyo haiko katika kufanyika kwa mkutano pekee, bali pia katika namna fursa zilizojitokeza zinavyotumiwa baada ya mkutano kumalizika.

"Kwa hiyo, babu, kushiriki kwa wajumbe kutoka nchi nyingi kulikuwa na maana gani?" mjukuu akauliza. Babu akajibu, "Ushiriki huo uliwapa viongozi nafasi ya kukutana, kubadilishana mawazo na kujadili masuala yenye maslahi ya pamoja. Zaidi ya hayo, mikutano kama hii inaweza kusaidia kujenga uelewa na kuimarisha uhusiano kati ya mabunge, ingawa manufaa yake ya muda mrefu hutegemea hatua zinazochukuliwa baada ya majadiliano."

Babu akaendelea kusimulia, "Nilipoendelea kuutazama mkutano huo katika ndoto yangu, nilivutiwa na namna viongozi walivyotumia nafasi hiyo kuendeleza mazungumzo nje ya vikao vya pamoja. Nilimwona Spika wa Bunge la Tanzania, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, akifanya mazungumzo ya pande mbili na viongozi wa mabunge mbalimbali, akiwemo kiongozi wa Bunge la Uingereza." Alieleza kwamba mazungumzo hayo yalionesha namna mkutano wa kimataifa unavyoweza kutoa nafasi ya kujadili masuala mahususi na kutafuta maeneo ya ushirikiano kati ya mabunge.

"Babu, mazungumzo hayo ya pande mbili yana umuhimu gani?" mjukuu akauliza. Babu akamjibu, "Ni sehemu ya kile kinachoitwa diplomasia ya kibunge. Hii ni njia ambayo wabunge na viongozi wa mabunge hutumia mazungumzo na mikutano kujenga uhusiano, kubadilishana uzoefu na kutafuta fursa za kushirikiana katika masuala ya maslahi ya pamoja." Akaongeza kwamba mikutano ya pande mbili, inayojulikana kwa Kiingereza kama bilateral meetings, inaweza kusaidia kutambua maeneo ya ushirikiano na kuweka msingi wa majadiliano yatakayoweza



kuendelezwa baadaye.

"Kwa hiyo, babu, Spika alikuwa akitekeleza wajibu wake wa kidiplomasia hata nje ya ukumbi wa mikutano?" mjukuu akauliza. Babu akajibu, "Ndiyo, mwanangu, kwa sababu diplomasia ya kibunge haipimwi kwa hotuba pekee, bali pia kwa fursa za ushirikiano zinazotokana na mazungumzo na hatua zinazofuata."

Babu akawatazama wajukuu wake na kuongeza, "Hili linaonesha umuhimu wa ushirikiano wa taasisi katika kuimarisha nafasi

ya Tanzania duniani. Rais, Bunge na Spika wana majukumu yanayotofautiana lakini yanayoweza kukamilishana katika kufungua fursa za kimataifa na kuzitumia kwa manufaa ya taifa."

"Babu, Bunge likimpongeza Rais, maana yake Serikali haiwezi tena kuulizwa maswali?" mjukuu mmoja akauliza. Babu akacheka na kujibu, "Hapana, mwanangu, pongezi na uwajibikaji vinaweza kwenda pamoja. Bunge linaweza kutambua mchango wa Rais katika mafanikio fulani na wakati huohuo kuendelea kutekeleza wajibu wake wa kikatiba wa kuisimamia Serikali."

"Ni kama mwalimu anavyoweza kumpongeza mwanafunzi kwa kufanya vizuri katika somo moja bila kuacha kumpima katika masomo



mengine," babu akaeleza. "Vivyo hivyo, kutambua mafanikio hakufuti wajibu wa Bunge wa kuuliza maswali na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali, kama ambavyo usimamizi huo haupaswi kumaanisha kupuuza mafanikio yaliyopatikana."

Baada ya mazungumzo hayo, babu aliendelea kusimulia ndoto yake. "Nilipotazama tena mandhari ya Arusha, nilijiuliza jinsi jiji hilo lingeweza kutumia uzoefu wa kuandaa mkutano mkubwa wa kimataifa ili kuvutia mikutano mingine na kuimarisha shughuli za kiuchumi." Aliona kwamba fursa hiyo ingeweza kuendelezwa kupitia uboreshaji wa miundombinu, huduma bora na mazingira yanayovutia uwekezaji.

"Lakini hilo halitatokea lenyewe," babu akasisitiza. "Linahitaji mipango madhubuti, uwekezaji endelevu na ushirikiano kati ya taasisi za umma na sekta binafsi." Alieleza kwamba mafanikio ya mkutano mmoja yanaweza kufungua milango ya fursa nyingine, lakini manufaa yake ya muda mrefu yanategemea hatua zinazochukuliwa baada ya mkutano.

Babu akakumbuka pia mjadala kuhusu ushiriki wa wanawake katika mkutano huo. "Katika hoja ya Azimio, ilielezwa kwamba wanawake wabunge walifikia asilimia 39.4 ya washiriki," alisema. "Takwimu hiyo inatukumbusha umuhimu wa ushiriki wa wanawake katika mijadala ya kibunge na kimataifa, ingawa ni muhimu kuzingatia taarifa rasmi kuhusu kundi la washiriki lililohesabiwa."

"Babu, je, mkutano uliishia kwenye hotuba na mazungumzo?" mjukuu akauliza. Babu akajibu, "Kulikuwa pia na Tamko la Arusha, ambalo umuhimu wake utategemea hatua zitakazochukuliwa kulitekeleza." Akaongeza kwamba matamko ya kimataifa yana thamani kubwa zaidi yanapofuatiliwa na kuhusishwa na hatua zinazoweza kuleta matokeo yanayopimika.

Babu akanyamaza kwa muda, kisha akasema, "Sasa ninaelewa kwa nini Azimio la Bunge lina maana pana zaidi ya pongezi. Linatoa nafasi ya kutambua mchango wa uongozi huku likitukumbusha umuhimu wa kutumia nafasi ya Tanzania katika jukwaa la kimataifa kuendeleza uhusiano na fursa zinazoweza kuwanufaisha wananchi."

"Lakini babu, wanasiasa wanaweza kuwa na maoni tofauti kuhusu Serikali," mjukuu mmoja akasema. Babu akajibu, "Ni kweli, mwanangu, na tofauti za kisiasa ni sehemu ya demokrasia. Kutofautiana kuhusu sera hakupaswi kuzuia kutambua mchango uliofanyika, kama ambavyo kupongeza mafanikio hakupaswi kuzuia kuuliza maswali kuhusu utekelezaji wake."

"Kwa hiyo, babu, mkutano huu unamaanisha kwamba Tanzania imeendelea?" mjukuu mdogo akauliza. Babu akamjibu, "Mkutano huu umeipa Tanzania nafasi ya kuonesha uwezo wake wa kuandaa matukio ya kimataifa na kuimarisha ushirikiano wa kibunge. Hata hivyo, maendeleo ya nchi hayawezi kupimwa

kwa tukio moja pekee, bali kwa namna fursa zinazotokana nalo zinavyogeuzwa kuwa manufaa yanayoonekana katika maisha ya wananchi."

Babu akaendelea, "Ningependa kuona fursa zilizojitokeza Arusha zikiendelezwa, uhusiano na mabunge mengine ukiimarishwa na uwezekano wa biashara na uwekezaji ukifuatiliwa. Rais, Spika, wabunge, watumishi wa umma na wananchi wana nafasi tofauti katika safari hii, lakini juhudi zao zinapokamilishana, heshima ya kimataifa inaweza kuwa msingi wa maendeleo ya kudumu."

Wajukuu walitulia, wakitafakari maneno ya babu. Kisha mjukuu mkubwa akauliza, "Babu, basi, funzo kubwa la ndoto yako ni lipi?" Babu akatabasamu na kujibu, "Azimio la Bunge ni kama mbegu iliyopandwa kwenye udongo wenye rutuba, lakini thamani yake huonekana zaidi inapolelewa hadi kuzaa matunda. Vivyo hivyo, pongezi hutambua mchango wa leo, huku uwajibikaji na ufuatiliaji vikisaidia kuhakikisha kwamba fursa za leo zinakuwa manufaa ya kesho."

Giza lilikuwa limeingia na wajukuu wakajiandaa kwenda kulala. Kabla hawajaondoka, babu akawaambia, "Tofauti za kisiasa zinaweza kuwepo, lakini hazipaswi kutuzuia kutambua mafanikio yanayostahili kuthaminiwa wala kutekeleza wajibu wa kuuliza maswali. Jambo la msingi ni kuhakikisha kwamba heshima ya Tanzania duniani inaambatana na hatua zinazowajibika na matokeo yenye manufaa kwa wananchi."

BUNGE LA TANZANIA NA DUNIA: MKUTANO WA 153 WA IPU NA FURSA YA KUBADILI DIPLOMASIA KUWA MAENDELEO

Athuman Hussein, *ndc*
a.brambati@bunge.go.tz

Katika uhusiano wa kimataifa, nafasi ya taifa haijengwi kwa sauti yake pekee, bali pia kwa uwezo wake wa kukutanisha mataifa mbalimbali, wadau, kuanzisha mazungumzo yenye tija na kubadilisha uzoefu kupitia uhusiano wa kimataifa wenye fursa za maendeleo. Katika juhudi hizo, diplomasia ya kibunge ina nafasi ya pekee. Kupitia mabunge yao, mataifa hujenga uhusiano, hubadilishana uzoefu, hujadili changamoto zinazofanana na hutafuta suluhisho la pamoja kwa masuala yanayovuka mipaka ya nchi.





Kwa Tanzania, kuandaa Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) ni fursa ya kuendeleza nafasi ya Bunge katika ushirikiano wa kimataifa na kuunganisha mazungumzo ya kibunge na vipaumbele vya maendeleo ya taifa. Umuhimu wa nafasi hii unaonekana pia katika msisitizo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika ujumbe wake kwa mkutano huo, alipobainisha:

"… Serikali yangu inaheshimu sana mamlaka hayo, ikitambua kwamba nafasi ya Bunge huimarisha kazi za Serikali na uwajibikaji tunaodaiwa kwa wananchi wa Tanzania…" Alisema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Kauli yake inasisitiza nafasi ya Bunge katika kuimarisha utawala bora na uwajibikaji kwa wananchi. Hata hivyo, mchango wa Bunge hauishii katika utungaji wa sheria na usimamizi wa Serikali, bali unajumuisha pia kujenga uhusiano na ushirikiano baina yake na mabunge mengine duniani kupitia mazungumzo, ushirikiano na kubadilishana uzoefu.

Katika muktadha huo, uenyeji wa Mkutano wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) unapata maana pana zaidi ya heshima ya kitaasisi. Ni fursa kwa Tanzania kutumia diplomasia ya kibunge kuimarisha uhusiano wa kimataifa, kutangaza uwezo wake na kutafuta njia za kuendeleza maslahi ya taifa.

Maana hiyo inadhihirika tunapoitazama Arusha, chini ya kivuli cha Mlima Meru, ikiwa kitovu cha mikutano na mazungumzo yaliyowaleta pamoja wabunge, maspika na viongozi kutoka sehemu mbalimbali za dunia. Kupitia mkutano huo, washiriki walipata nafasi ya kubadilishana uzoefu, kujadili changamoto zinazofanana na kujenga uhusiano unaoweza kuendelezwa hata baada ya mkutano.

Wakati mazungumzo hayo yakifungua milango ya ushirikiano wa kimataifa, shughuli za mkutano ziliweka pia mazingira ya fursa za kiuchumi katika mji mwenyeji. Hoteli, migahawa, kampuni za usafiri na wafanyabiashara wengine walinufaika na mahitaji ya wageni, huku utamaduni na vivutio vya Tanzania vikipewa nafasi ya kufahamika zaidi kimataifa.

Hivyo, uenyeji wa Mkutano wa 153 wa IPU, uliofanyika Arusha kuanzia tarehe 5 hadi 9 Oktoba 2026, unapaswa kutazamwa kwa upana unaozidi idadi ya wajumbe waliohudhuria na shughuli zilizotekelezwa. Thamani yake ya muda mrefu itategemea namna Tanzania itakavyotumia uhusiano uliojengwa na fursa zilizojitokeza kuimarisha diplomasia ya kibunge na kuchochea maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Lakini, je, tukio hili lina maana gani zaidi ya mikutano, hotuba na picha za pamoja? Kwa nini Mtanzania wa kawaida, mkazi wa Arusha,

mfanyabiashara, mwanasiasa, msomi na mtumishi wa umma anapaswa kulitambua kama jambo lenye umuhimu kwa taifa?

Majibu ya maswali haya yanapatikana katika dhana ya diplomasia ya kibunge, ambayo inaunganisha mazungumzo ya kisiasa na fursa za ushirikiano wa kimataifa. Kwa mtazamo huo, uenyeji wa mkutano huu haukuwa tu jukumu la kuratibu hafla ya kidiplomasia, bali pia fursa ya kuimarisha uhusiano wa kimataifa, kukuza uchumi na kuendeleza nafasi ya Tanzania katika jumuiya ya kimataifa.

Kwa muda mrefu, diplomasia imehusishwa zaidi na Serikali, mabalozi na wizara zinazoshughulikia mambo ya nje. Hata hivyo, mabunge nayo ni washiriki muhimu katika kujenga uelewano na ushirikiano kati ya mataifa. Kupitia Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), ulioanzishwa mwaka 1889, wabunge hupata jukwaa la kujadili masuala ya amani, demokrasia, utawala bora, haki za binadamu na maendeleo endelevu.

Katika majadiliano hayo, wabunge hawawakilishi taasisi zao pekee, bali pia maslahi na matarajio ya wananchi wanaowawakilisha. Hivyo, mazungumzo yanayofanyika katika majukwaa ya kibunge yanaweza kufungua njia za kubadilishana uzoefu, kujenga uelewano na kutafuta suluhu za changamoto zinazofanana kati ya mataifa.

Hapo ndipo maana ya Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huu inapozidi ukubwa wa ukumbi wa mikutano. Bunge la Tanzania lilipata fursa ya kuwakutanisha wawakilishi wa mataifa mbalimbali nchini, kushiriki katika mijadala ya kimataifa na kuonesha uzoefu wake wa kibunge. Ushirikiano na uhusiano uliojengwa katika mazingira hayo, unaweza kuendelezwa kupitia ushirikiano wa Kamati za Bunge, kubadilishana utaalamu na mazungumzo ya baadaye.

Mbali na fursa za kitaasisi, uenyeji wa Mkutano wa 153 wa IPU uliipa Tanzania jukwaa la kujitambulisha kwa dunia. Kupitia Arusha, wageni walikutana na utamaduni, huduma, biashara na ukarimu wa Watanzania. Kwa namna hiyo, taswira ya taifa haikujengwa na hotuba za viongozi pekee, bali pia na uzoefu wa wageni walipokutana na watu, taasisi na mazingira ya nchi.

Hata hivyo, taswira ya taifa haidumu kwa namna wageni walivyopokewa pekee, bali kwa kile kinachofuata baada ya kuondoka. Uhusiano ulioanzishwa unahitaji kuendelezwa, fursa zilizobainika zinahitaji kufuatiliwa na maarifa yaliyopatikana yanahitaji kutumika. Kwa kufanya hivyo, heshima ya kimataifa itageuka kuwa mtaji wa uhusiano wenye thamani ya muda mrefu.

Katika uga wa uchumi, mikutano ya kimataifa huchochea mahitaji ya malazi, maakuli, usafiri, mawasiliano na huduma nyingine. Mahitaji hayo yanaweza kufungua milango kwa hoteli, migahawa, madereva, waongoza watalii, wafanyabiashara wadogo na wa kati pamoja na watoa huduma za kitaalamu. Kwa Arusha, fursa hizo zinaweza kuimarisha nafasi ya jiji hilo katika utalii wa mikutano na kuitangaza zaidi Tanzania kama mahali pa kutembelea, kufanya biashara na kuwekeza.



Fursa hizo zinakuwa pana zaidi zinapounganishwa na utalii wa mazingira, wanyamapori, utamaduni na urithi wa kihistoria. Mgeni anayefika kwa shughuli ya kitaasisi anaweza kuvutiwa kurejea kwa mapumziko au kuitangaza Tanzania kwa wengine. Hata hivyo, mvuto wa tukio moja hautoshi kujenga manufaa ya kudumu. Natija ya matukio ya aina hiyo, inahitaji kuwepo kwa huduma

bora, bidhaa zenye ushindani na mikakati ya kuendeleza mawasiliano baada ya mkutano.

Kwa msingi huo, mafanikio ya kiuchumi hayapaswi kupimwa kwa idadi ya wageni au gharama za kuandaa mkutano pekee. Inafaa pia kutazama biashara za ndani zilizonufaika, ajira zilizochochewa, huduma zilizonunuliwa nchini na uhusiano wa kibiashara unaoweza kuendelea. Tathmini ya namna hii ndiyo inayoweza kutenganisha mafanikio ya kuandaa tukio na mafanikio ya kubadili tukio kuwa fursa ya maendeleo.

Lakini manufaa ya mkutano hayapo katika uchumi pekee. Kwa wananchi, diplomasia ya kibunge ina maana pale maarifa na uzoefu



unaopatikana katika majukwaa ya kimataifa vinasaidia kuboresha utungaji wa sheria, usimamizi wa fedha za umma na ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera. Uzoefu wa mabunge mengine katika elimu, afya, ajira, mazingira, usawa na ushiriki wa vijana huibua mawazo mapya katika mijadala ya kitaifa.

Hata hivyo, kujifunza kutoka kwa wengine hakumaanishi kuiga kila wanachofanya. Sanaa ya maendeleo ni kuchota maarifa duniani na kuyapa sura inayolingana na mahitaji ya nyumbani. Kwa hiyo, jukumu la Bunge ni kuchambua uzoefu huo, kutathmini uhalisia wake na kubaini mbinu zinazoweza kuimarisha mifumo na maisha ya Watanzania.

Kwa wabunge, mkutano unatoa somo kuhusu umuhimu wa uwakilishi unaoambatana na kujifunza, kujenga mitandao na kubadilishana uzoefu. Kwa Serikali, unaonesha nafasi ya kudumisha na kuendeleza uhusiano wa kimataifa katika kutafuta ushirikiano wa biashara, uwekezaji, elimu na maendeleo. Kwa wasomi, unafungua eneo la kuchunguza uhusiano kati ya diplomasia ya kibunge, utawala bora na maendeleo, huku kwa wafanyabiashara ukikumbusha umuhimu wa kubadili uhusiano kuwa fursa halisi.

Kwa wanasiasa, tukio hili pia linaibua funzo muhimu: maslahi ya taifa yanaweza kuendelezwa kupitia mazungumzo na ushirikiano hata pale mitazamo inapotofautiana. Kwa watumishi wa umma, linakazia umuhimu wa kuratibu taasisi, kuhifadhi maarifa na kuyatumia katika kuboresha utendaji. Kwa vijana, linatoa picha ya dunia ambayo fursa zake zinaweza kufikiwa kwa maarifa, ubunifu, ujuzi na uwezo wa kujenga uhusiano wenye tija.

Pamoja na fursa hizo, ni muhimu kuwa na uelewa wa uhalisia kwamba uenyeji wa mkutano hauleti moja kwa moja uwekezaji, mikataba mipya au ustawi wa wananchi. Matokeo hayo yanahitaji mipango inayotekelezeka, taasisi zinazowajibika na mifumo ya kufuatilia maendeleo yaliyopatikana. Vivyo hivyo, uhusiano unaojengwa unahitaji kudumishwa na maarifa yaliyokusanywa yanahitaji kusambazwa kwa taasisi zinazoweza kuyatumia.

Katika hayo, tofauti kati ya kufanikisha mkutano na kujenga urithi wake inapatikana. Kwa Bunge la Tanzania, urithi huo unaweza kuwa katika kuimarisha uwezo wa kidiplomasia, kuboresha uratibu wa mikutano ya kimataifa na kuendeleza ushirikiano na mabunge mengine. Kwa Arusha, unaweza kuwa fursa ya kuimarisha nafasi yake katika utalii wa mikutano, huku kwa sekta binafsi ukiwa mwanzo wa uhusiano mapya ya kibiashara.

Ili fursa hizo zisiishie kuwa kumbukumbu nzuri, kila mdau anapaswa kuwa na nafasi katika hatua inayofuata. Serikali inaweza kufuatilia maeneo ya ushirikiano yaliyojitokeza, sekta

binafsi ikaendeleza uhusiano wa kibiashara na taasisi za elimu na utafiti zikachambua mafunzo yaliyopatikana. Bunge nalo linaweza kuendeleza mawasiliano ya kibunge na kuhakikisha kuwa uzoefu wenye manufaa unafikishwa kwa wahusika wanaoweza kuutumia.

Kwa hiyo, kipimo cha mwisho cha mafanikio hakitakuwa tu namna mkutano ulivyoandaliwa, bali pia kile kitakachobaki baada ya pazia lake kushuka. Kwa mwanasiasa, ni namna heshima ya kimataifa inavyotumika kuendeleza maslahi ya taifa; kwa msomi, ni namna matokeo yanavyopimwa kwa ushahidi na kwa mwananchi, ni kama fursa zinazotokana na uhusiano huo zitachangia ustawi wa jamii. Mitazamo hii inakutana katika swali moja kuu: "Tutafanya nini ili fursa ya leo iwe manufaa ya kesho?"

Kwa mtazamo mpana, uenyeji wa Mkutano wa 153 wa IPU unatoa nafasi ya kutafakari namna Bunge linavyoweza kuwa daraja kati ya wananchi na dunia, kati ya mazungumzo ya kisiasa na fursa za kiuchumi na kati ya maarifa ya kimataifa na mahitaji ya ndani. Ni fursa ya kuitangaza Tanzania, kuimarisha uhusiano na kujifunza kutoka kwa wengine. Hata hivyo, thamani yake ya kudumu itategemea namna fursa hizo zitakavyofuatiliwa na kugeuzwa kuwa matokeo yenye manufaa kwa taifa.

Kwa maana hiyo, kuhitimishwa kwa mkutano hakumaanishi mwisho wa safari, bali mwanzo wa hatua ya kutafsiri fursa zake kuwa matokeo. Wageni wanaweza kurejea katika nchi zao na kumbi za mikutano kurejea katika shughuli zake za kawaida, lakini uhusiano ulioanzishwa haupaswi kufifia pamoja na kumbukumbu za tukio. Badala yake, yanapaswa kuwa msingi wa ushirikiano endelevu, maarifa yanayotumika na fursa zinazofuatiliwa kwa manufaa ya pande zote.

Changamoto inayobaki ni kugeuza heshima ya kuwa mwenyeji wa dunia kuwa urithi wenye manufaa kwa taifa. Jambo hilo linahitaji kuimarishwa kwa uhusiano, kufuatiliwa kwa fursa zilizobainika na kuanza kutumika kwa maarifa yaliyopatikana ili kujenga ushirikiano wenye tija na kuchochea maendeleo.

Kwa mantiki hiyo, dunia ilikutana Tanzania, sasa ni zamu ya Tanzania kuonesha thamani ya mkutano huo kupitia hatua zitakazofuata. Matarajio yaliyosisitizwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu matumizi ya uzoefu uliobadilishanwa na majadiliano yaliyofanyika yanatoa msukumo wa kutazama mbele, ili mkutano usibaki kuwa kumbukumbu ya tukio la kimataifa, bali uwe chachu ya manufaa ya kudumu kwa mataifa na wananchi wake.

Hatimaye, mafanikio ya diplomasia ya kibunge hayatapimwa kwa hadhi ya kuwa mwenyeji pekee, bali kwa uwezo wa kugeuza mazungumzo kuwa ushirikiano, uhusiano kuwa fursa na fursa kuwa maendeleo yanayogusa maisha ya Watanzania.




SPEAKER - URT
VVIP
PRESIDENT IPU
IPU153 ASSEMBLY
PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA


1889







PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S. L. P. 941,
40490 Tambukareli,
DODOMA
Simu: +255 26 2322761-5
Fax No. +255 26 2324218
E-mail: cna@bunge.go.tz